epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
0745 700710
LIKE & FOLLOW US
Jumatatu Oktoba 7, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

ISSN 0856 • Na. 0581822
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital



UKURASA 22
## CARVAJAL AIPA PIGO MADRID

UKURASA WA 2
## KATIBU MKUU CCM AMPIGIA SIMU WAZIRI AKATATUE KERO

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Balozi Dk. Emmanuel Nchimbi jana...

UKURASA WA 4
## MAT WAMLILIA PROF. SHAO, MWANAMAGEUZI WA TIBA NCHINI

MADAKTARI wamesema aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya KCMC na Makamu...

UKURASA WA 5
RIPOTI MAALUM -3
## TB SUGU JANGA KWA VIJANA WA KIUME NCHINI

WATAALAMU wa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) wanasimulia namna TB ilivyo changamoto...

## Mji wakosa maji kwa wiki tatu
UKURASA 8

BINTI WA YOMBO
# ‘Afande’ kizimbani
UKURASA 2



Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini, IGP Camillus Wambura, akizungumza na maofisa, wakaguzi na askari wa vyeo mbalimbali mkoani Kigoma jana, ikiwa ni mwendelezo wa ziara yake ya kikazi katika mikoa ya Kanda za Kipolisi. **PICHA: JESHI LA POLISI**



## Kigogo CHADEMA ashinda uchaguzi akiwa mahabusu
UK.4

**MICHEZO** SIMBA NA BAJETI YA BIL. 28/- 2024-25 UK.24

**KATUNI** UK.6

### SAKATA BINTI WA YOMBO

# 'Afande' kupanda kizimbani leo

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

FATMA Kigondo anayetuhumiwa kuwatuma vijana kumbaka kwa kundi na kumwingilia kinyume cha maumbile binti mkazi wa Yombo Dovya, jijini Dar es Salaam, leo anatarajiwa kufikishwa kupanda kizimbani katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Dodoma kujibu mashtaka yanayomkabili.

Septemba 5, mwaka huu, mahakama hiyo iliahirisha shauri lililofunguliwa na Wakili Paul Kisabo dhidi ya Afande Fatma kutokana na hakimu aliyekuwa anasikiliza shauri hilo kuhamishwa kituo cha kazi huku shauri hilo likiwa halijapangiwa hakimu mwingine.

Kesi hiyo ilipangwa kusikilizwa Septemba 5 mwaka huu katika mahakama hiyo mbele ya Hakimu Mkazi Fransis Kishenyi, afande huyo akikabiliwa na shtaka kuwasaidia wahalifu kutenda kosa la ubakaji kwa kundi.

Akizungumza nje ya mahakama hiyo baada ya kuahirishwa kwa shauri hilo, Wakili Kisabo aliyefungua mashtaka hayo dhidi ya afande huyo, alidai ni kuhamishwa kituo cha kazi kwa hakimu aliyepangiwa kesi.

"Lakini leo kama mlivyoona, mshtakiwa tayari amefikishwa mbele ya mahakama na kusomewa mashtaka yanayomkabili," alidai wakili huyo.

Katika kesi namba 23476 ya mwaka 2024 ya ubakaji kwa kundi na kumwingilia kinyume cha maumbile iliyokuwa ikisikilizwa na Hakimu Mkazi wa Mahakama hiyo, ilitolewa hukumu yake Septemba 30 mwaka huu.

Katika hukumu hiyo washtakiwa wote walikutwa na hatia na kuhukumiwa kifungo cha maisha gerezani na kutakiwa kulipa Sh. milioni moja kila mmoja.

Waliohukumiwa kifungo hicho ni pamoja na aliyekuwa askari wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), MT 140105, Clinton Damas, maarufu Nyundo, aliyekuwa askari Magereza C.1693 Praygod Mushi, Nickson Jackson, maarufu Machuche na Amin Lema, maarufu Kindamba.

Wote kwa pamoja walikuwa wanakabiliwa na mashtaka ya kubaka kwa kundi na kumwingilia kinyume cha maumbile binti wa Yombo Dovya, jijini Dar es Salaam aliyetambulishwa kwa jina la XY.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA KUU DODOMA**

**SHAURI LA ARDHI NA. 5555 YA 2024**

**VALENCE CYRIL URIO ..............................................MDAI**

**DHIDI YA**

1. **DODOMA CITY COUNCIL**
2. **THE ATTORNEY GENERAL**
3. **THE COMMISSIONER FOR LANDS, MINISTRY OF LANDS......WADAIWA HOUSING HUMAN SETTLEMENTS**
4. **ADAM MUSSA MBEGA**

**KWA: ADAM MUSSA MBEGA**

**POPOTE PALE ALIPO**

**YAH: TAARIFA YA KUSIKILIZWA KWA SHAURI LA ARDHI NA. 5555 YA 2024 MAHAKAMA KUU YA TANZANIA DODOMA.**

UNAFAHAMISHWA KWAMBA; Shauri tajwa hapo juu litasikilizwa Mahakama kuu ya Tanzania Dodoma mbele ya **MHE. J. L. MASABO, JAJI** wa Mahakama kuu ya Tanzania Dodoma , saa tatu (3:00) kamili asubuhi siku ya Jumanne tarehe 5/11/2024.

HIVYO; Unatakiwa Ufike wewe wenyewe au Wakili wako siku hiyo iliyotajwa bila kukosa .

**NA ENDAPO;** Hautafika wewe au wakili wako siku hiyo iliyotajwa inatosha kumaanisha kwamba shauri hili litashughulikiwa na Mahakama kama itakanyoamua pasipo wewe au wakili wako kuwepo.

**IMETOLEWA;** Kwa mkono wangu na Mhuri wa Mahakama leo hii tarehe 2/10/1024.

NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU DODOMA




Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa (kushoto), akizungumza na watumishi wilayani Kigamboni kwenye ukumbi wa Chuo cha Maendeleo ya Wananchi, jana ikiwa ni ziara yake ya kikazi mkoani Dar es Salaam. **PICHA: OWM**

# Katibu Mkuu CCM ampigia simu waziri akatatue kero

**Na Halfani Chusi,** SIMIYU

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Balozi Dk. Emmanuel Nchimbi jana alimpigia simu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohamed Mchengerwa kutaka ufafanuzi wa lini soko na stendi vitajengwa Lamadi, mkoani Simiyu.

Balozi Dk. Nchimbi, akiwa katika siku ya kwanza ya ziara yake ya siku saba mkoani Simiyu, wakati akihutubiwa wananchi katika mkutano wa hadhara, alielezwa kero kuu zinazowasumbua na kuwakwamisha kwenye utekelezaji wa majukumu yao.

Akitoa ufafanuzi huo, Waziri Mchengerwa alisema: "Rais Samia Suluhu Hassan amezingatia malalamiko hayo na alituelekeza kuhakikisha eneo hilo zinapelekwa fedha za ujenzi wa soko na ujenzi wa barabara.

"Lakini pia kwa kuwa kuna ukimya tutakuwa hapo (Lamadi) kuanzia mwezi ujao kuona namna gani tutakwenda kufanya maboresho kwa sababu fedha tulionayo kwa sasa ni ya ujenzi wa soko la kisasa na barabara kwa kiwango cha lami urefu wa kilomita nane," alisema Mchengerwa.

Aliongeza kuwa wataalamu watakaokwenda, wataangalia uwezekano wa kufanya tathmini na kuongeza ujenzi wa stendi na kwamba kuanzia mwezi ujao wanategemea kutangaza zabuni ya kuanza ujenzi wa soko la kisasa na barabara.

Aliwahakikishia wananchi wa Lamadi kwamba changamoto zao zitatatuliwa na suala la stendi amelichukua na wanaangalia uwezekano wa kulijumuisha wakati wa ujenzi wa soko na barabara.

Akikata simu ya Mchengerwa, Balozi Dk. Nchimbi alirusha dongo kwa vyama vya upinzani kwamba havina mipango thabiti ya kuongoza nchi.

"Kiongozi madhubuti anazungumzia mipango ya kuongoza nchi.

Lakini vyama vya upinzani wakipata nafasi wanazungumza maandamano, kuchana kanga na kuzomea.

"Viongozi wa CCM wanaandaliwa, hakuna kiongozi ndani ya chama atakaa miaka 40. CCM kitaendelea kuwa chama kijana zaidi kwani kina viongozi vijana na wazee wenye kuwalea vyema," alisisitiza.

Alitoa wito kwa wananchi hao kuendelea kushirikiana na CCM, akisisitiza chama hicho kimeendelea kuonesha nia njema katika kuwatumikia wananchi.

Kuhusu Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Vijiji na Vitongoji unaotarajiwa kufanyika mwishoni mwa mwezi ujao, Katibu Mkuu alitoa rai kwa wananchi kujitokeza kwa wingi, akitamba kuwa chama chake kitateua wagombea wenye kujali changamoto za wananchi na si maslahi binafsi.

"Ikifika muda wa kujiandikisha, tujitokeze kwa wingi kujiandikisha katika Daftari la Wakazi kuanzia Septemba 11 hadi 20, 2024 ambalo litahusika katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa Novemba 27, 2024. Daftari la Kudumu la Wapigakura ni kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu 2025," alibainisha.

Katika hatua nyingine, Balozi Dk. Nchimbi alisema CCM itachangia Sh. milioni mbili kuunga mkono ujenzi wa vituo vya madereva bodaboda katika Mji wa Lamadi baada ya kundi hilo kulalamika linateseka na jua wakati wa kutafuta ridhiki.

Katibu wa NEC Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa CCM Taifa, Amos Makalla alisema mkoa wa Simiyu ni wa 18 kufanya ziara za kikazi na kukagua utekelezaji ilani na kusikiliza kero za wananchi.

Mbunge wa Busega, Simon Lusengekile alisema eneo lake lina changamoto ya viboko na tembo kuvamia makazi ya wananchi na kuharibu rasilimali zao na kuomba serikali iruhusu wavunwe ili wananchi wanaozunguka ziwa, wawe salama.

Balozi Dk. Nchimbi alimwahidi kulifikisha suala lake kwa Waziri wa Maliasili na Utalii, Balozi Dk. Pindi Chana ili changamoto vyhiyo itafutiwe ufumbuzi.

Kada wa CCM aliyejiengua akitokea Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Peter Msigwa alisema Tanzania iko salama chini ya uongozi wa chama hicho na kwamba wanaodhani vyama vya upinzani vitawaletea maendeleo, wafumbue macho kwa kuwa vyama hivyo vimebaki kile alichokiita kulialia.

Katibu wa NEC Siasa na Uhusiano wa Kimataifa, Rabia Abdallah Hamid aliwataka vijana kujituma na kufanya kazi za kuwaingizia kipato, akiwahimiza kuchangamkia fursa ya mikopo ya asilimia 10 inayotarajiwa kuanza kutolewa muda wowote kuanzia sasa.

TANGAZO

# UJIO WA FIC UMEKUWA MKOMBOZI KWA JAMII NA MAKUNDI YA WAHITAJI

F.I.C
FOOTBAL INVESTMENT COMPANY

FIC si jukwaa la uwekezaji tu; bali pia ni nyenzo kuu ya ustawi wa umma. Kama jukwaa linalolenga kuboresha maisha ya Watanzania kupitia njia za kifedha, FIC inajibu kikamilifu wito wa mashirika ya kimataifa kusaidia kupunguza changamoto za kiuchumi zinazowakabili Watanzania wengi.

Umoja wa Mataifa na mashirika mengine ya kimataifa yameanzisha miradi mingi ya misaada nchini Tanzania, ikijumuisha maeneo kama vile huduma za afya, afya na ufufuaji uchumi. Ujio wa FIC unawapa wananchi njia nyingine thabiti ya kupata uhuru wa kiuchumi—kupata maendeleo binafsi kupitia uwekezaji.

Hisia yetu ya uwajibikaji wa kijamii inatuchochea kusaidia zaidi jamii masikini kuondokana na matatizo yao. Upendo hauna thamani, na upendo unapaswa kushirikishwa.

FIC inaamini kwa dhati kwamba jitihada za ustawi wa jamii hazitakoma kamwe. Tutaendelea kuleta mabadiliko chanya katika jamii na kushirikiana kuunda mustakabali bora wa siku zijazo.







# Kigogo CHADEMA ashinda uchaguzi akiwa mahabusu

Na Mwandishi Wetu

ALIYEKUWA Meya wa Kinondoni, Boniface Jacob, ameshinda nafasi ya Mwenyekiti wa Kanda ya Pwani ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kwa kupata kura 60, sawa na asilimia 77, akiwa mahabusu gerezani.

Akitangaza matokeo hayo, Katibu wa Kanda ya Pwani, Kerenge Jerry alisema mshindani wake wa karibu, Gervas Lyenda alipata kura 17 sawa na asilimia 23. Wengine waliochaguliwa ni Mwenyekiti wa Baraza la Wazee CHADEMA (BAZECHA), James Haule, Makamu Mwenyekiti, Wilson Katunzi, huku Katibu akichaguliwa Deogratius Kajula.

Mwekahazina ni Florence Kasilima, Mwenyekiti Baraza la Wanawake CHADEMA (BAWACHA), Joyce Mwabamba, Makamu Mwenyekiti, Husna Masoud, huku Katibu akichaguliwa Evangelina Marcel na Mwekahazina, Grace Mgonjo.

Kwa upande wa Baraza la Vijana CHADEMA (BAVICHA), Mwenyekiti ni Juma Juma, Katibu Lilian Byebalilo na Mwekahazina, Alex Daniel.




Wananchi pamoja na wanafunzi wa shule za msingi na sekondari katika kata ya Mwendakulima, Halmashauri ya Manispaa ya Kahama wakiwa kwenye matembezi ya kuhamasisha lishe bora huku wakiwa na bango lenye ujumbe wa Lishe Bora kwa Maendeleo ya Taifa jana. **PICHA: SHABAN NJIA**

# Madaktari wamlilia Prof. Shao, mwanamageuzi wa tiba nchini

Na Salome Kitomari

MADAKTARI wamesema aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya KCMC na Makamu Mkuu wa kwanza wa Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira mstaafu, Prof. John Shao (80), ameacha alama kubwa.

Akimzungumzia Prof. Shao aliyefariki jana hospitalini KCMC, Rais wa Chama cha Madaktari Tanzania (MAT), Dk. Mugisha Nkoronko, alisema ameacha alama kubwa na isiyofutika katika sekta ya afya kukiwa na mageuzi makubwa, ikiwamo idadi kubwa ya madaktari wabobezi. Alisema kuwa Prof. Shao alikuwa miongoni mwa madaktari wa kwanza kusoma shahada ya magonjwa ya vimelea mbalimbali, akiwa mkufunzi katika Chuo Kikuu cha Tiba Muhimbili.

"Ni mwanamageuzi wa sekta ya afya, alishiriki mageuzi wakati tunaingia katika mpango wa kuruhusu sekta binafsi kuendesha shughuli za kijamii ikiwamo afya. Baada ya sheria kupitishwa kuruhusu sekta binafsi kuwekeza mwaka 1995 ndio walikuwa wa kwanza kuanzisha chuo kikuu binafsi cha kwanza cha Tumaini na Chuo Kikuu cha Tiba, Kitivo cha KCMC akiwa mkuu wa chuo wa kwanza," alisema.

Aliongeza: "Akiwa Mkurugenzi wa KCMC, tulishuhudia alisomesha madaktari, madaktari wote unaowaona leo walishawishiwa na yeye kusomea ubingwa na ubobezi walionao sasa hivi. Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), Dk. Peter Kisenge ni matunda ya dhati ya Prof. Shao," alisema rais huyo.

Alisema kuwa Prof. Shao alianzisha Kituo cha Utafiti (KCRI), ambacho alikianzisha kwa kushirikiana na wadau, akianzisha pia maabara ya bayoteknolojia, iliyoshirikI katika utafiti wa udhibiti wa malaria duniani chini ya Mpango wa Bill & Melinda Gate.

"Ameacha alama nyingi katika afya, ukiona taasisi ya tiba za njia ya mkojo pale KCMC ni yeye, huwezi kuitaja bila kumtaja Prof. Shao. Uchunguzi wa magonjwa ya tumbo kwa kutumia kamera maalum inayomezwa ni yeye," alisema.

Pia alisema ameshiriki utafiti wa matibabu ya kifua kikuu (TB) kwa kushirikiana na Hospitali ya Rufani ya Taifa ya Magonjwa Ambukizi Kibong'oto, mkoani Kilimanjaro na alianzisha kliniki shirikishi ya VVU na Ukimwi kwa familia. Dk. Mugisha alisema kwa kushirikiana na viongozi wengine, walisababisha kukawa na CT Scan ya kwanza kwa Kanda ya Kaskazini.

"Pia alishirikii mageuzi ya kisera na kimuundo, alifanikisha uanzishwaji Mpango wa Elimu ya Madaktari (MEPI), ndio kiini cha ushirikiano baina ya Chuo Kikuu cha Duke Marekani na KCMC, na Chuo Kikuu Radbound Nijmegen cha Uholanzi.

Taarifa ya tanzia iliyotolewa kwa umma jana na Katibu Mtendaji wa Shirika la Msamaria Mwema (GSF) na Mkurugenzi Mtendaji wa KCMC, Prof. Gileard Masenga, ilieleza kuwa Prof. Shao alikutwa na umauti jana Oktoba 6, 2024. Prof. Shao alizaliwa mwaka 1944, ni mtanzania wa kwanza kuwa na shahada ya magonjwa ya vimelea vya magonjwa mbalimbali, aliwahi kuwa mkufunzi katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam mwaka 1978-1981, Mshauri wa wanafunzi UDSM kuanzia 1981-1986, Profesa Mshiriki mwaka 1982-1990 na Profesa tangu 1986.

Tangu mwaka 1994, alikuwa Katibu Mkuu wa Shirikisho la Umoja wa Madaktari Afrika, mwaka 1992 alikuwa mjumbe wa Kamati ya Mabadiliko ya Sekta ya Afya Tanzania na Rais wa Chama cha Madaktari Tanzania mwaka 1990-1992.

**Bwana alitoa na Bwana ametwaa. Jina la Bwana lihimidiwe.**


## HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA

HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA
THE CITY COUNCIL OF DODOMA
CCD

## TANGAZO LA MRADI WA VIWANJA ENEO LA KIKOMBO KITALU "DA" NA "N"

MKURUGENZI WA HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA ANAWATANGAZIA WANANCHI WOTE AMBAO HAWAJAKAMILISHA MALIPO YA UNUNUZI WA VIWANJA KATIKA MRADI WA VIWANJA ENEO LA KIKOMBO KATIKA KITALU "DA" NA "N" KUWA WANATAKIWA KUKAMILISHA MALIPO YOTE NDANI YA SIKU KUMI NA NNE (14) KUANZIA TAREHE 3 HADI 16 OKTOBA, 2024.

KUSHINDWA KUKAMILISHA MALIPO HAYO; KIWANJA HICHO KITATOLEWA KWA MWOMBAJI MWINGINE BILA TAARIFA ZAIDI KWAKO NA WEWE UTAREJESHEWA FEDHA YAKO BAADA YA KUKATWA ASILIMIA 10 KWA GHARAMA ZA USUMBUFU.

**TANGAZO HILI LIMETOLEWA NA MKURUGENZI WA JIJI LA DODOMA**

RIPOTI MAALUM -3

# TB sugu janga kwa vijana wa kiume

## -Muhimbili yapokea mtoto miaka miwili

Na Romana Mallya

**Katika sehemu ya pili ya ripoti hii jana, kulikuwa na simulizi za wagonjwa wa kifua kikuu (TB) mgodini na hali ilivyo katika Hospitali ya Kibong'oto. Endelea na sehemu ya mwisho ya ripoti hii:**




Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Ndani Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Dk. Verdiana Byemelwa, akizungumza katika mahojiano maalum na Nipashe kuhusu TB sugu. **PICHA: ROMANA MALLYA**

WATAALAMU wa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) wanasimulia namna TB ilivyo changamoto kwa vijana wa kiume, huku kundi kubwa la wanaoonwa zaidi hospitalini huko likiwa la wanaofanya kazi migodini.

Katika mazungumzo maalum na Nipashe, Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Ndani MNH, Verdiana Byemelwa, anasema takwimu za hospitali hiyo ya hadhi ya juu zaidi kitaifa zinaonesha wagonjwa wanaolazwa na wanaohudhuria kliniki, wengi wao ni wa jinsia ya kiume.

Anasema kuwa kwa mwezi Agosti mwaka huu, walikuwa na wagonjwa 21 wenye TB sugu. Kati yao, vijana ni 14 (wa kike saba).

Mtaalamu huyo anataja sababu ya vijana kuwa katika hatari ya maambukizi hayo ni mizunguko mingi waliyonayo kila siku na ni kundi ambalo halipendi kutibiwa.

Anasema vijana ni kundi ambalo hupenda kukaa wengi eneo moja; mfano chuoni, baa au migodini ambako ni miongoni mwa eneo hatarishi kwa ugonjwa huo.

Dk. Verdiana anasema kuwa kati ya waliowatibu mwaka huu, mmoja tu alirejea hospitalini huko baada ya kupata maambukizi, ambaye alikuwa katika tiba ya miezi tisa na hakuna kifo.

Akizungumzia TB kitaalamu, Dk. Verdiana anasema ni ugonjwa wa mapafu unaosababishwa na kimelea kinachoitwa Mycobacterium Tuberculosis (MTB), ambacho huathiri mapafu na sehemu nyingine za mwili kama mifupa, moyo, ubongo, tumbo na njia ya mkojo.

Anaeleza kuwa ugonjwa wa TB sugu uko wa aina mbili ukichangiwa na usugu wa dawa moja, dawa mbili au tatu.

Mtaalamu huyo anasema watu wanapata TB sugu kutokana na kushindwa kudhibiti maambukizi kutoka kwa mtu mmoja kwenda kwa mwingine ambaye hajapata matibabu au hajagundulika kuwa na tatizo hilo.

"Mgonjwa kukaa miaka mitatu bila kutumia dawa yoyote inayostahili kutibu maradhi yake, huchangia kimelea hujibadilisha na kupata usugu," anasema.

Usugu mwingine, daktari huyo anasema huchangiwa na watu kutomaliza dozi ambapo kwa mgonjwa wa TB ya kawaida, hutakiwa kutibiwa kwa miezi sita au zaidi kwa aina nyingine ya TB, lakini baadhi ya watu hunywa dawa chini ya muda huo na kuacha na wengine hunywa kwa kuruka siku.

Pia anasema wagonjwa ambao hawatatibiwa vizuri, wanaporudi katika jamii huwa na vimelea sugu na huambukiza wengine.

"Sababu nyingine ya usugu huchangiwa na mtindo wa maisha na kufanya vimelea vibadilike kuwa sugu," anasema.

Dk. Verdiana pia anasema usugu mwingine husababishwa na mtu kutumia dawa anazonunua bila ushauri wowote wa daktari.

"Ukiwa na mgonjwa, mlete hospitalini na mwambie hatakiwi kutibiwa kwa dawa za kienyeji. Tuwaambie dawa zinachukua muda gani ili kusaidia matibabu kuwa rahisi," anashauri.

### WALIO HATARINI

Kuhusu watu walio katika hatari ya kupata TB sugu, Dk. Verdiana anasema ni wenye upungufu wa kinga mwilini, wakiwamo wazee, wagonjwa wa kisukari na wenye Virusi vya Ukimwi (VVU) na wagonjwa wa saratani.

Kundi lingine lililoko hatarini kwa mujibu wa mtaalamu huyo wa Muhimbili ni watoto chini ya miaka mitano kwa kuwa kinga za mwili hazijakomaa.

Dk. Verdiana anasema wagonjwa ambao wanaoonwa zaidi hospitalini huko wenye TB sugu ni walio na VVU na watu wanaofanya kazi migodini, kundi ambalo nalo wanalitaja lipo hatarini zaidi kupata maambukizi kutoka na shughuli mbalimbali zinazofanyika huko.

Mtaalamu anasema dawa zipo za kutosha na matibabu sahihi ya TB sugu huanzia miezi tisa hadi miezi 18 na huduma hizo hutolewa bila malipo.

Anasema dawa ya TB sugu inayotumika kwa sasa Tanzania yenye matumaini makubwa na kupunguza kutibu kutoka miezi 18 mpaka 24 na kurudi miezi tisa ni Bedaquiline, ambayo imeonesha matokeo makubwa kwa wagonjwa.

Dk. Verdiana anasema changamoto wanazokutana nazo katika kuwahudumia ni mapokeo ya wagongwa wengi, hawaamini kama kweli wana TB sugu na hawapendi kukaa hospitalini.

"Wapo wenye TB sugu na wana magonjwa mengine ambayo matibabu yake yanakwenda nje ya TB sugu, huitaji kulipia, sasa wagonjwa wanakuwa hawataki kulipia, wanafikiri matibabu yote ni bure.

"Kwa mfano mgonjwa anakuwa na TB sugu na ana kisukari, matibabu ya kisukari mfano dawa zake, sasa mgonjwa anataka vyote vilipwe na hospitali.

"Hivyo, baadhi ya ndugu huondoka na hutuachia wagonjwa. Serikali hulipa gharama za TB, lakini magonjwa mengine yaliyojitokeza kwa mgonjwa wa TB yanayopaswa kulipiwa na mgonjwa hajalipa, hospitali huingia gharama," anasema.

Kwa mwaka wa fedha 2021/22, kiasi cha fedha kilichotumika kwa wagonjwa wote wa msamaha waliotibiwa Muhimbili - Upanga ni Sh. bilioni 19, 2022/23 Sh. bilioni 18 na 2023/24 Sh. bilioni 13.

Dk. Verdiana anaendelea kusema wagonjwa wengi wa TB sugu hujificha kwa kuhofia unyanyapaa kwa kuona wakisema watakaa hospitalini miezi mitatu na nyumbani kutengwa kuanzia vyumba, vyombo mpaka vijiko.

Dk. Verdiana anasema Shirika la Afya Duniani (WHO) kupitia ripoti yake ya mwaka 2020 linaonesha Tanzania ni miongoni mwa nchi sita za Afrika zenye idadi kubwa ya wagonjwa wa TB. Nchi zingine ni pamoja na Ethiopia, Kenya, Namibia na Afrika Kusini.

"Kwa Tanzania, mwaka 2020 wagonjwa 26,800 waliripotiwa kufariki dunia kwa TB. Kwa dunia nzima, Tanzania ipo nafasi ya 15 kwa nchi ambazo zina maambukizi ya TB.

### MTOTO AGUNDULIKA TB SUGU

Mratibu TB na Ukoma Muhimbili, Dk. Nuru Msanga, anasema kuwa mwaka 2021 walipokea mtoto wa miaka miwili mwenye TB sugu.

"Aliletwa Muhimbili akionekana kama ana dalili za shida ya kupumua, alikuwa na shida ya moyo, kinga zake ni ndogo na alikuwa na maambukizi ya VVU.

"Akalazwa na baadaye aliingizwa Chumba cha Uangalizi Maalum (ICU), alipopimwa ndipo ikabainika ana TB sugu," anasema.

Dk. Msanga anasema kwa sasa wagonjwa wenye TB sugu walioko Muhimbili wakijumlisha na wale wanaokuja kwa ajili ya matibabu wapo 21. Wenye TB ya kawaida idadi yao ni zaidi ya 200.

"Ukiongeza na kituo chetu cha IDC kwa wenye TB ya kawaida ni wagonjwa kati ya 400 mpaka 500, lakini kwa TB sugu wapo 21 kwa sasa," anafafanua.

Mei 13, mwaka huu, aliyekuwa Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, alisema wataendelea kusimamia utoaji huduma za TB na ukoma kwa mujibu wa Mpango Mkakati wa Sita (2020/21 - 2025/26) wa kupambana na magonjwa hayo.

Alisema serikali imetenga Sh. bilioni 84.864 ili kufanikisha mpango huo ikiwamo ununuzi wa vifaa tiba, vitendanishi na dawa za kutibu.

Alitaja malengo makuu ya mpango huo ni kupunguza maambukizi mapya ya TB kwa asilimia 50, kupunguza vifo kwa asilimia 75.

"Hadi kufikia mwezi Machi, mwaka huu, Tanzania imepunguza maambukizi mapya ya TB kwa asilimia 36, kutoka wagonjwa 306 kwa kila watu 100,000 mwaka 2015 hadi wagonjwa 195 kwa kila watu 100,000 mwaka 2023.

"Takwimu zinaonesha vifo vitokanavyo na TB vimepungua kwa asilimia 67 kutoka vifo 56,000 mwaka 2015 hadi vifo 18,000 mwaka 2023 na hivyo kuwa kwenye njia sahihi ya kufikia lengo la kupunguza maambukizi kwa asilimia 50 na vifo kwa asilimia 75 pindi ifikapo mwaka 2025," alisema.

Ummy alisema katika kipindi hicho jumla ya wagonjwa 194 wa TB sugu waligundulika na kuanzishiwa matibabu ambao ni sawa na asilimia 43 ya lengo la kugundua wagonjwa 453, kulinganishwa na wagonjwa 266 waliogundulika katika kipindi kama hicho mwaka 2022/23 sawa na asilimia 40 ya lengo la kuibua wagonjwa 664 wa TB sugu.

MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Waamuzi acheni woga wa kuongeza dakika soka lichezwe kwa dakika 90

**KATIKA** mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara kati ya Simba na Coastal Union, uliochezwa Ijumaa iliyopita kwenye Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam, kuliibuka mzozo kwa wachezaji kumzonga mwamuzi kwa kitendo chake cha kumaliza mpira wakati wakiamini ulikuwa unastahili dakika zaidi za kuendelea kucheza.

Hali hiyo ilisababisha tafrani kidogo, ambapo alizongwa na wachezaji wa pande zote mbili pamoja na mabenchi yao ya ufundi, kila upande ulionekana kutoridhishwa na namna mpira ulivyomalizika, wote wakiamini dakika zilipaswa kuongezwa kutokana na matukio mbalimbali yaliyosababisha mpira kusimama na kutochezwa kwa dakika zote 90.

Coastal Union wao waliona kama shambulizi lao limezimwa kwa makusudi kwani walikuwa wanagongeana kwenda langoni mwa Simba.

Simba nao waliona dakika zilikuwa bado, walizihitaji kwa kile walichoona wangeweza kupata bao la tatu katika mchezo huo uliomalizika kwa sare ya mabao 2-2.

Nipashe tunaona uhitaji huo wa dakika kwa timu zote mbili unaweza kuanza kuwaamsha waamuzi wengi wa Kitanzania hasa wa akiba ambao wana matatizo ya kutotunza muda kwa usahihi.

Katika mchezo huo, Coastal Union walionekana kupoteza dakika nyingi kwa makusudi baada ya kurudisha mabao mawili.

Kwa bahati nzuri wao walijua hilo, lakini baadaye walizihitaji baada ya kuona kuwamudu wapinzani wao, Simba ambao nao walijua Coastal walipoteza sana muda, hivyo waliuhitaji ili wasake bao la ushindi.

Tatizo la kuongezwa dakika chache ambazo hazina uhalisia kwa sasa limeonekana kuota mizizi kwenye soka la Tanzania.

Kwanza kabisa ni nadra sana kuona zimeongezwa dakika tano kipindi cha kwanza. Mara nyingi kipindi cha kwanza ndicho huongezwa dakika chache zaidi hata kama mpira ulisimama kwa dakika tano kutokana na matukio tofauti uwanjani, lakini kwa Ligi Kuu nchini, waamuzi huongeza dakika mbili au tatu tu.

Kipindi cha pili ndiyo angalau unaweza kuona zimeongezwa nne, zikizidi sana tano. Hii imekuwa ni kama utaratibu au kanuni za waamuzi wa Ligi Kuu na haijulikani wao wanaendeshwa na kanuni zipi tofauti zile za Shirikisho la Soka duniani (Fifa), ambazo zinataka kuhakikisha mechi inachezwa ndani ya uwanja kwa dakika 90.

Hata kama kutakuwa na mapumziko ya kunywa maji, wachezaji kuumia na ucheleshwaji wa muda makusudi, lakini bado baadhi ya waamuzi hapa nchini wamekuwa hawaongezi dakika stahiki zilizopotea.

Kwa sasa Ulaya tunaona, zinaongezwa kuanzia dakika tano mpaka 10, kutegemea na upotezwaji wa muda. Hii yote ni kutaka mpira uchezwe ndani ya uwanja kwa dakika zote 90 na si chini ya hapo.


Kule Ulaya wanapoongeza mpaka dakika 10, timu huwa hazipotezi muda, cha kushangaza hapa nchini ambapo timu zinazoitwa au kujiita ndogo zikicheza na Simba au Yanga, halafu zikiwa na uhakika fulani tu kama mechi hii kushinda ama kupata sare kunakuwa na vituko vya wachezaji kujilaza makusudi, makipa kujifanya wameumia hadi kuvua 'gloves' na viatu, lakini mwamuzi mtunza muda ataongezwa tatu au nne tu.

Lakini pia waamuzi wa ndani nao wamekuwa waoga kuongeza dakika baada ya zile za nyongeza hata kama zilizoongezwa mpira hazikukamilika kwa mpira kuchezwa uwanjani kutokana na upotezwaji huo wa muda.

Sisi tunaona ifike wakati sasa waamuzi waondoe woga, wachezeshe kwa dakika zote 90 kwa mujibu wa kanuni za Fifa. Hata zikiongezeka dakika 10, kama refa atachezesha kwa haki na kufuata sheria za soka tunaamini hakuna matatizo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Adam Fungamwango

## Muungwana Lazima Nilonge

# Ngao ya Jamii kumalizika bila kujua ligi itaanza lini ni kituko

**NIWAPE** kwanza hongera timu ya JKT Queens kwa kutwaa Ngao ya Jamii baada ya kuifunga Yanga Princess bao 1-0, katika mchezo wa fainali uliopigwa Jumamosi Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam.

Kwa jinsi walivyocheza wakianza kwa kutoa kipigo kizito cha mabao 7-0 dhidi ya Ceasiaa Queens katika mchezo wa nusu fainali walionekana kustahili ubingwa huo.

Ikumbukwe mwaka jana JKT Queens ilifungwa kwenye hatua ya fainali kwa mikwaju ya penalti 5-4 na Simba Queens, baada ya sare ya bao 1-1.

Msimu huu Simba Queens ilitolewa hatua ya nusu fainali na watani zao wa jadi, Yanga Princes kwa mikwaju ya penalti 4-3, baada ya sare ya bao 1-1.

Baada ya hongera, nitoe pongezi pia kwa timu zote nne zilizoshiriki michezo hiyo ya nusu fainali, fainali na kusaka mshindi wa tatu kwa kutoa burudani kwa mashabiki ambao walikuwa wakimiminika kwenye uwanja huo uliopo Mwenge Dar es Salaam, kwa ajili ya kuangalia michezo hiyo.

Wakati michezo hiyo inapigwa, nilifuatilia na kugundua kuwa hakuna taarifa yoyote ya ratiba ya Ligi Kuu ya Wanawake mpaka sasa.

Hata Kocha Msaidizi wa Ceasiaa Queens, Shabani Zanziba, alisikika akisema baada ya Ngao ya Jamii kutakuwa tena na mapumziko kabla ya kuanza ligi hiyo.

Cha kujiuliza mpaka sasa ni kwa nini hakuna ratiba yoyote ya Ligi Kuu ya Wanawake, wakati mechi za Ngao ya Jamii zimechezwa.

Maana ya Ngao ya Jamii, ni kuashiria kuanza kwa msimu mpya wa ligi kokote kule, lakini hii imekuwa kinyume chake.

Imeonekana kama Ngao ya Jamii ni kama michuano tu ambayo inajitegemea na haiashirii chochote kile.

Kwa upande wa soka la Wanaume tunaona kuwa ikichezwa Ngao ya Jamii tayari ratiba ya Ligi Kuu nayo inakuwa imeshatoka.

Msimu huu baada ya kumalizika kwa Ngao ya Jamii tu, Agosti 11 kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Yanga ilipoichukua kwa kuifunga Azam FC mabao 4-1, siku tano baadaye tu, yaani Agosti 16, Ligi Kuu Tanzania Bara ikaanza.

Sijajua tatizo ni nini, lakini kama hali ni hivi, nadhani kusingekuwa na haraka ya kuanza mechi za Ngao ya Jamii. Nadhani ingesubiriwa hadi mipango ya ligi hiyo ikae sawa.

Kwa maana hiyo, klabu zilikusanya wachezaji na kuwaweka kambini kwa ajili ya michezo miwili tu ya Ngao ya Jamii, na baada ya hapo zitalazimika kuvunja kambi hadi hapo zitakapopata taarifa ya kuanza kwa Ligi Kuu.

Hakuna kitu kingine unachoweza kukiita, ila ni usumbufu na kituko. Huu ulikuwa ni wakati wa wachezaji kuendelea kukaa kambini na kujifua kwa ajili ya kujiandaa na ligi. Ikumbukwe kuwa hakuna klabu yoyote inayoweza kuwaweka kambi wachezaji eti ikijiandaa na Ligi Kuu ambayo haijuu itachezwa lini, labda JKT Queens tu.

Na hiyo ni kwa sababu yenyewe ni timu ya jeshi, ambayo muda wote wapo kambini na mazoezi ni kama kazi za kawaida tu, na hawana tatizo la gharama.

Kwa klabu zingine kwa kuepuka gharama zitawaacha wachezaji waende makwao mpaka watakapowaita tena. Baadhi yao ni wachezaji kutoka nje ya nchi, hivyo watarejea makwao wakati tayari walikuwa wameshafika kwenye maeneo ya kazi.

Ifike wakati sasa wahusika, Shirikisho la Mpira wa Miguu nchini (TFF), chini ya vitengo vyake zinavyosimamia soka la wanawake kuangalia hili.

Wanapaswa kuandaa Ngao ya Jamii ambapo tayari wameshajiandaa na Ligi Kuu ya Wanawake na si hivi ilivyotokea msimu huu.

# Waziri, RC wapongeza CRDB kuongeza ujumuishi kifedha

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA jitihada za kusogeza huduma jirani na kuwajumuisha wananchi kiuchumi, Benki ya CRDB imezindua matawi mawili, hivyo kutanua zaidi mtandao wake nchini.

Matawi hayo mapya yamezinduliwa katika Halmashauri ya Mpimbwe, mkoani Katavi na Wilaya ya Kilolo, mkoani Iringa, hivyo kufikisha zaidi ya matawi 260 yaliyomo nchini kote na kuifanya Benki ya CRDB kuongoza kwa mtandao mkubwa wa matawi yanayotoa huduma.

Akizindua tawi la Majimoto mkoani Katavi, Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Geophrey Pinda, alisema mwishoni mwa wiki kuwa ni furaha kubwa kwa wana Mpimbwe kuona benki yao ya kizalendo ya CRDB ikiwasogezea huduma ili kuwapa fursa zitakazowasaidia kukuza kipato chao binafsi na kuchangia zaidi katika uchumi wa taifa.

"Ninazipongeza sana juhudi zenu za kuwafuata wananchi mahali walipo kwani hii ni ishara tosha kuwa Benki ya CRDB imejipanga vilivyo kuunga mkono jitihada za serikali kufanikisha mipango na mikakati ya kuwajumuisha Watanzania wengi katika mfumo rasmi wa huduma za fedha," alisema Pinda.

Mbunge huyo wa Kavuu alisema fedha ni kichocheo muhimu cha maendeleo ya taifa, hivyo ukuaji wa sekta hiyo ni muhimu katika kukuza uchumi na kupunguza umaskini nchini.

Alisema kuwa ili sekta ya fedha itoe mchango unaokusudiwa, inapaswa iwe imara na yenye uwezo mkubwa wa kuwafikia wateja mahali walipo, iwe mijini au vijijini.

"Ninafahamu mwezi uliopita mlikuwa hapa mkitoa elimu ya fedha kupitia programu yenu ya Imbeju. Kwa wananchi wa kawaida ambao wengi ni wafanyabiashara wanahitaji programu kama hizi ili kuwapa elimu itakayowasaidia kukuza biashara zao.

"Endeleeni kuwaelimisha wananchi lakini wekeni na usimamizi utakaowawajibisha wanufaika kurudisha mitaji waliyoichukua," alisisitiza Pinda.

Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Peter Serukamba, alisema wananchi wa Iringa wanajishughulisha na kilimo pamoja na biashara, hivyo kuhitaji huduma za benki kwa usalama wa fedha zao.

"Mkoa wa Iringa unachangia kwa kiasi kikubwa kulilisha taifa letu, nafaka mpaka nyanya na vitunguu vinatoka hapa. Mazao haya yote na mengine yanalimwa na wakulima wadogo ambao wanahitaji huduma za benki ili kutunza fedha wanazozipata.

"Ujio wa Benki ya CRDB hapa Ilula utakuwa na mchango mkubwa kwa uchumi wa mwananchi mmojammoja na halmashauri pia," alisema Serukamba.

Akizungumza kuhusu uzinduzi wa matawi hayo mawili, Mkurugenzi wa Wateja wa Awali na wa Kati wa Benki ya CRDB, Bonaventura Paul alisema kuwa kwa kipindi cha miaka 28 sasa, mtandao wao wa huduma umetanuka kutoka matawi 19 yaliyokuwapo mwaka 1996 mpaka zaidi ya matawi 260.

Hizi zote, Mkurugenzi Paul alisisitiza ni juhudi za kusogeza huduma karibu zaidi na watanzania wa mjini na vijijini. "Katika Mkoa wa Katavi, Benki yetu ya CRDB ilikuwa na tawi moja tu la Mpanda. Tumeongeza la pili pale Majimoto na mengine yanakuja hivi karibuni.

"Iringa tulikuwa na matawi matatu na sasa yamefika manne, tutaendelea kusogeza huduma zetu kwa wananchi kadri itakavyoonekana inahitajika," alisema Paul.

Benki hiyo pia inatoa huduma kupitia CRDB Wakala ambapo kwa Mkoa wa Katavi, ina mawakala 171 wakiwamo 39 wanaotoa huduma katika Halmashauri ya Mpimbwe, huku Iringa kukiwa na mawakala 686 wakijumuisha 16 waliomo wilayani Kilolo.

"Mawakala hawa hutoa huduma karibu zote kwa wateja kama ilivyo wakienda katika matawi ya benki yetu. Kutokana na kuongezeka kwa mahitaji ya wateja, benki yetu iliona kuna umuhimu wa kuboresha huduma ili kuendana na mahitaji yaliyopo sasa na yatakayojitokeza baadaye katika maeneo ya Majimoto na Ilula.

"Baada ya kufanya utafiti wa kina, Benki ilijenga matawi hayo ili kuwahudumia wananchi wa maeneo husika na vitongoji jirani," alisema Paul.

Benki pia ilikabidhi mifuko 50 ya saruji yenye thamani ya Sh. milioni moja kwa ajili ya ujenzi wa mabweni ya wasichana wanasoma katika Shule ya Sekondari Kiheka iliyoko Ilula, Mkurugenzi Paul akiahidi kuipa Sh. milioni moja taslimu kwa ajili ya kugharamia ujenzi.



Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Ndege (ATCL), Ladislaus Matindi akimkabidhi cheti cha uhudumu ndani ya ndege mmoja wa wahitimu wa chuo cha shirika hilo mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

## VACANCY ANNOUNCEMENT

**Job Title: SECURITY ADVISORS (2 POSITIONS- FIELD BASED)**
**Job Type:** Full Time
**Reports to:** Construction Security Lead and Security Manager
**Location:** Along the EACOP Pipeline Route

### WHO WE ARE

The East African Crude Oil Pipeline (EACOP) project is a Midstream development located across Uganda and Tanzania that includes a nearshore Marine Storage and Export Terminal (MST). Once completed, the EACOP Company will operate the East African Crude Oil Pipeline, a 1,443 km long, electrically heated crude oil export pipeline that transports oil from Kabaale - Hoima in Uganda, to the Chongoleani Peninsula near Tanga Port in Tanzania for crude export to the international markets.

### JOB DIMENSIONS/ GENERAL JOB DESCRIPTION

**To be responsible for:**

- Supporting the EACOP Security Manager, ensuring security plans for all site locations within Lot 2/3 are in place and fit for purpose.
- Ensuring effective monitoring of all contractor's security infrastructure, plans, policies, and procedures are implemented across all site locations in Lot 2/3 to required standards / KPIs.

### DUTIES & RESPONSIBILITIES

**In accordance with policies and procedures in place in EACOP, The Warehouse & Stock Officer is responsible for:**

- Assist the Lot 2&3 Construction Security Lead in conducting risk assessments, security vulnerability assessment, audits of sites, routes, airports, and accommodation in accordance with EACOP standards visiting all MCPY, AGI and PPL sites within lot 2/3 regularly to observe CONTRACTORS, Subcontractor's security providers performance.
- Ensure that all project sites are covered by robust Level 1 CONTRACTORS, Subcontractor's security plans, and ensure that Focal Point Plans are maintained.
- Ensure the in-country POB is kept up to date with all locations and contact details and where applicable support contractors in the implementation of security plans policies and procedures.
- Interface with EACOP Site Representatives and attend all preconstruction and construction meetings, addressing any security concerns that may be raised. As directed by the Lot 2&3 Construction Security Lead or the EACOP Security Manager.
- Conduct regular training, and exercises or coordinating with others to conduct training as needed.
- Assist with inductions to all new arrivals in country. Promote and educate all new arrivals on the Security System.
- Address any security concerns that are raised by the EACOP management team.
- Conduct meetings and audits of EACOP CONTRACTOR Security subcontractors to ensure they are appropriate and fit for purpose.
- Assist with the review of EACOP CONTRACTORS, Subcontractor's security plans and KPIs.
- Work in different sites in multiple cities as and when required, and as instructed by the Lot 2&3 Construction Security Lead or EACOP Security Manager.
- Assist the Lot 2&3 Construction Security Lead and or the EACOP Security Manager in responding to Security incidents or events.
- Monitor all media sources for any security related incidents in Uganda 24/7. Incident database to be maintained.
- Identify potential risks that may have an adverse effect on the project and ensure that they are captured on the security risk register.
- Advise senior project management on any security related concerns in the absence of the Lot 2&3 Construction Security Lead and coordinate any Security events that occur.
- Work within a multi-cultural business framework and provide ethical and compliant support.
- Mentor exemplary behavior regarding HSE, Ethics and EACOP "Code of Conduct" policy.

### HEALTH, SAFETY & ENVIRONMENTAL RESPONSIBILITIES

**EACOP is committed to ensuring that the health, safety and welfare of workers, communities, and the environment are well addressed and managed. Therefore, the employee is mandated to:**

- Fully complies with Company H3SE (Health, Safety, Social, Security & Environment) policies and Life Saving Rules.
- Actively participates in HSEQ and promotes this culture to co-workers.
- Remain vigilant and maintain continuous awareness of potential unsafe conditions.
- Communicates to management any HSE related concerns and ways to improve them.
- Maintains a workplace & workspace that is safe, clean, and always neat – practice good housekeeping.

### QUALIFICATIONS / EXPERIENCE REQUIRED

**Academic Qualifications:**

- Bachelor's degree or above in related security risk management.
- 5 years' experience in security and/or emergency management related field.
- Previous experience required in similar role and/or industry (project specific) related field.
- Strong interpersonal skills and ability to communicate well in English language, verbal and written.

**Experience Required:**

- Strong verbal and written communication skills (including analysis, interpretation, & reasoning)
- Ability to multi-task and prioritize.
- Able to act independently without instruction in high pressure situations.
- Ability to use MS Office (word, excel, Outlook) competently and to a high standard.
- Attention to detail and high level of accuracy in record keeping.
- A high level of integrity and understanding of the requirement for all project personnel to follow approved procedures.
- Analytical and problem-solving skills.
- Ability to work well autonomously and within a team in a fast-paced and deadline-oriented environment.
- Knowledgeable, familiar, and commensurate experience with the HSE operating environment.
- An 'Incident Free' mind-set, and be a role model for their project team (Direct/Indirect hires)
- Excellent teamwork & skills being able to work with the various sub-teams to resolve issues and reach decisions that are in the best interests of the integrated project team.

### HOW TO APPLY

The applicant must submit his/her Curriculum Vitae CV and a Cover Letter explaining why he/she is the suitable candidate for the position. Applicants are also required to provide details of three (3) referees one of whom should be the most recent employer. **Please submit your application only through ANY of the contact information provided below. Application deadline is 31st October 2024.**

**Air Swift:** airswift.com
**CCL:** tanzania@cclglobal.com
**IMI:** imi-tanzania@imi-eag.com
**ITM:** recruitmenttanzania@itmafrica.com
**Qsourcing:** recruitmenttanzania@qsourcing.com
**Seaowl:** sestz@seaowlgroup.com

**NOTE: No payment is required at any stage of the recruitment process.**

# Wananchi wapaza sauti ukosefu wa maji

**Na Mwandishi Wetu,** LINDI

WANANCHI wa mji wa Lindi wameeleza adha ya ukosefu wa maji kwa takribani wiki tatu ambayo imesababisha watumie muda mwingi kutafuta huduma hiyo.

Mji huo unategemea maji kutoka vyanzo vya Kitunda, Mmongo na Liwayawaya na kiasi kinachopatikana huko kimeshindwa kukidhi mahitaji.

Mwandishi wa habari hizi alitembelea baadhi ya maeneo na kubaini yaliyokumbwa na kadhia hiyo ni pamoja na Mitema, Banduka Kata ya Rasbura, Mlandege, Sabasaba Kata ya Jamhuri.

Wakizungumzia kadhia hiyo, Salima Yusufu, Juma Daudi, Hemedi Saidi na Ezekiel Mathias walidai kuwa kwa zaidi ya wiki tatu sasa hawajapata huduma hiyo kutoka Mamlaka ya Majisafi, Salama na Mazingira Mji wa Lindi (LUWASA).

"Tangu Septemba Mosi hadi leo (juzi) Oktoba 5, hatujapata maji katika maeneo yetu," walidai.

Walisema kuwa licha ya serikali kujenga mradi mkubwa wa maji kutoka chanzo kilichoko kata ya Ng'apa na viongozi kuahidi kukamilika kwake kutakuwa ni mwarobaini wa tatizo hilo kwa mji wa Lindi, hali inaonekana chanzo hicho kutokuwa mkombozi kwa wananchi.

Baadhi ya viongozi wa Mitaa hiyo, Justin Mrope (Mitema), Ally Yusufu (Sabasaba) na Daud Juma (Banduka), wakizungumza kwa niaba ya wenzao, walisema walishakwenda mamlaka husika kutaka kufahamu tatizo linalochangia kukosa maji kwenye mitaa yao kwa muda mrefu.

"Ni kweli tulifika LUWASA kufahamu tatizo, lakini tumeelezwa sababu za umeme, kuharibika bomba linalopeleka maji kwetu na kupungua maji katika chanzo cha Ng'apa," walisema.

Mwandishi alipowasiliana na Mkurugenzi Mtendaji LUWASA, Juma Soud alithibitisha kuwapo tatizo hilo na kueleza linatarajia kutatuliwa ndani ya muda mfupi baada ya mkandarasi kupata vifaa.

"Ni kweli tatizo hilo limechukuwa muda mrefu kutokana na mkandarasi kuchelewa kupata vifaa, lakini sasa tayari kati ya kesho au keshokutwa vitakuwa vimewasili," alisema Soud.

# Serikali yapiga marufuku NGO za nje kuhoji wananchi

**Na Faustine Feliciane aliyekuwa** SHINYANGA

SERIKALI imepiga marufuku taasisi binafsi za kimataifa zinazoingia nchini bila kufuata sheria na kufanya kazi, ikiwa pamoja na kuwahoji wananchi kuhusu mambo mbalimbali yanayofanyika.

Kauli hiyo imekuja siku chache baada ya taasisi moja ya nje ya nchi kuchapisha taarifa zikielezea ukiukwaji haki za binadamu katika Mgodi wa Dhahabu wa Barrick North Mara.

Akizungumza mkoani Shinyanga mwishoni mwa wiki, Naibu Waziri wa Madini, Dk. Steven Kiruswa, alisema Tanzania inaongozwa kwa mujibu wa Katiba na taratibu mbalimbali, hivyo taasisi na mtu yeyote kutoka nje anayetaka kuingia nchini kufanya kazi, ikiwamo kufanya uchunguzi wa kitu chochote, anatakiwa kufuata taratibu kupata idhini kutoka mamlaka husika.

Alisema NGO nyingi za kimataifa zimekuwa zinaingia nchini kinyemela na kuhoji wananchi juu ya mambo mbalimbali, hasa yanayohusu haki za binadamu na kwenda kuchapisha alichokiita "uongo kwa maslahi yao binafsi na kuichafua Tanzania".

"Taasisi zinazoona kuna ukiukwaji haki za binadamu na zinataka kuja kuhoji wananchi wetu, ni lazima zifuate utaratibu, kuja kimyakimya ni kinyume cha sheria na serikali hatuwezi kulivumilia jambo hilo, si rukhsa na ni marufuku kufanya hivyo," alionya Dk. Kirusa.

Naibu Waziri huyo alisema wananchi wanapaswa kuzikataa NGO zinazokwenda kuwahoji kwa kuwa zinakwenda kuchafua sifa ya Tanzania kimataifa.

"Wananchi msitoe ushirikiano kwa taasisi hizi zenye nia ovu na taifa letu, wanakuja kwa ajili ya kujinufaisha wao na si wananchi, wanatoa taarifa za uongo ambazo zinalichafua taifa letu.

"Migodi hii ya Barrick inaendeshwa kwa ubia na serikali, kuichafua (migodi hii), unaichafua serikali. Hatuwezi kufumbia macho, kila kitu katika migodi hii kinafanyika kwa kuangalia maslahi mapana ya wananchi wanayoizunguka, hakuna ukiukwaji wowote wa haki za binadamu na wananchi wamekuwa wanashirikishwa kwenye mambo mbalimbali," alisema.

Rais na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Migodi ya Barrick, Mark Bristow alisema migodi hiyo inaendeshwa na Watanzania na wamekuwa wanawashirikisha wananchi katika miradi mbalimbali ya maendeleo.

Alisema wanaozungumza juu ya ukiukwaji haki za binadamu katika Mgodi wa North Mara, wana nia ovu kwa kuwa wana nafasi ya kuuliza na kupewa maelezo ya ukweli, lakini hawafanyi hivyo.

Hivi karibuni, taasisi moja ya kimataifa ilitoa taarifa za madai ya kuwapo ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu katika Mgodi wa North Mara ulioko Tarime, mkoani Mara, jambo ambalo serikali na uongozi wa mgodi huo ulikanusha.



Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Omariy Kipanga (wa tatu kushoto), Mbunge wa Arusha Mjini, Mrisho Gambo (katikati) na Mkurugenzi Mkuu wa Oryx Gas Tanzania, Benoit Araman (wa pili kulia), wakiangalia namna mmoja wa walimu wa jijini Arusha anavyopika kwa kutumia gesi wakati wa maadhimisho ya Siku ya Walimu yaliyofanyika jijini humo juzi. Jumla ya majiko 5,000 ya Oryx yaligawiwa kwa walimu bure. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Marekani yahakikishia Tanzania kufadhili miradi ya maendeleo

**Na Mwandishi Wetu,** LINDI

MAREKANI kupitia Shirika lake la Maendeleo ya Kimataifa (USAID), imehakikishia Tanzania kuwa itaendelea kusaidia programu zenye kuleta matokeo muhimu nchini.

Kauli hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki na Mkurugenzi wa USAID nchini, Craig Hart aliyefanya ziara ya siku moja mkoani Lindi na kutembelea programu zinazofadhiliwa na shirika hilo.

Akitembelea mradi wa USAID Afya Yangu Kusini, Mkurugenzi huyo wa USAID aliambatana na Dk. Marina Njelekela, Mkurugenzi wa Mradi huo pamoja na Dk. Beatrice Christian, Naibu Mkurugenzi.

Mradi wa USAID Afya Yangu Kusini ni wa miaka mitano (Novemba 2021 hadi Novemba 2026) ambao unasimamiwa na Deloitte Consulting Limited pamoja na washirika wenza MDH na T-MARC na kutekelezwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, vituo vya afya, mashirika ya kiraia na mashirika ya kiimani (FBO).

Ni mpango huo unaolenga kusaidia Serikali ya Tanzania kupitia Wizara ya Afya na Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kutoa huduma bora za kinga na matibabu ya Virusi vya Ukimwi (VVU) na kifua kikuu (TB), hasa kwa vijana na watoto kupitia mbinu ya kina inayozingatia mteja na kuleta matokeo bora ya afya.

Mradi wa USAID Afya Yangu Kusini unatoa msaada wa kiufundi na nyenzo/au msaada wa kiutawala na usimamizi kwa Serikali ya Tanzania kupitia Wizara ya Afya na Ofisi ya Rais - TAMISEMI kupitia Mamlaka za Serikali za Mitaa, vituo vya afya vya umma na binafsi, na huduma za jamii na mashirika ya kidini ili kuongeza uwezo wao wa kusimamia na kutoa huduma bora za VVU/TB.

Akizungumza wakati wa ziara hiyo, Mkurugenzi wa Misheni ya USAID, Craig Hart, alisema USAID itaendelea kusaidia programu zenye kuleta matokeo muhimu katika Mkoa wa Lindi na kusaidia juhudi za Serikali ya Tanzania katika kuboresha upatikanaji huduma bora za afya mkoani humo.

Alipotembelea Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Lindi (Sokoine), Hart alizungumzia msaada wa USAID kwa miaka mingi na huduma, zikiwamo zinazosaidiwa na USAID Afya Yangu (Mradi wa Kusini). Alikubali uwezo wao wa kudhibiti ufadhili wa moja kwa moja pamoja na kuonesha mpango endelevu wa eneo/ramani ya barabara na kile ambacho kimeafikiwa kufikia sasa.

Pia alitembelea Kituo cha Matunzo na Tiba katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa na kukutana na Vijana Rika wa Jamii (Vijana wa Sitereki) ambao wanafanya uundaji wa mahitaji kupitia mijadala ya vikundi vidogo na mjadala mmoja mmoja katika jamii.

USAID Afya Yangu Kusini ndiyo washirika wakuu wa Utekelezaji wa afua za VVU na TB mkoani Lindi. Mkoa wa Lindi una jumla ya vituo vya afya 263 katika halmashauri sita.

USAID Afya Yangu Kusini inasaidia vituo vya afya 98 kati ya 130 vinavyotoa huduma za matunzo na tiba katika halmashauri zote sita zinazosaidiwa.

USAID Afya Yangu Kusini inajitahidi kufikia maeneo matatu ya matokeo ya kati ambayo ni: Kuboresha upatikanaji wa huduma bora za VVU/TB zinazomlenga mteja; kuboresha uwezo wa watu kufanya tabia nzuri ya kutafuta afya; na kuimarishwa kwa mazingira wezeshi kwa utoaji huduma bora za VVU/TB.





## HABARI KASKAZINI



Katibu wa Chama cha Walimu Tanzania (CWT), Muheza, mkoani Tanga, Seleman Mashaka (kushoto), akimkabidhi kipeperushi mwalimu wa Shule ya Sekondari ya Cheif Mang'enya, Ramadhani Msoroka (kulia), chenye mwongozo wa chama hicho. Wa pili kushoto ni Mwenyekiti wa CWT wilaya, Mashauri Kanyama. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Vikundi vidogo vya kifedha 700 vyainuliwa kiuchumi

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

SHIRIKA la Floresta Tanzania, limeanza kupata matokeo chanya katika miradi yake ya kilimo endelevu, baada ya kufanikiwa kuziinua jamii za vijijini zenye uhitaji kupitia programu mbalimbali za ukuaji wa kiuchumi na katika kilimo biashara cha mboga, matunda na viungo.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi wa Programu wa shirika hilo, Dafrosa Samagwa, mbali na kilimo endelevu, wametengeneza na kujenga uwezo wa kujiinua kiuchumi kwa vikundi vya huduma ndogo za fedha 700, huku sekta ndogo ya kilimo hai ikiwa imeanzisha na kujenga uwezo kwa vikundi vya mkondo maji 707.

Akizungumza katika Manispaa ya Moshi, mkoani Kilimanjaro, wakati wa maonyesho ya mbegu yaliyoandaliwa na Floresta Tanzania, kwa kushirikina na Shirika la World Vegetable Center, Samagwa, alisema katika miradi ya kilimo endelevu wanafanya kazi hiyo wilaya sita za mkoa huo.

Alisema sekta ndogo ya uzalishaji wa mboga, imeanza kuvutia makundi mbalimbali ya vijana kujihusisha na shughuli za uzalishaji kwa njia ya mkondo maji.

Alisema katika Wilaya ya Siha, Floresta imeunda vikundi 131 vya uzalishaji kwa njia ya mkondo maji katika Mto Sanya, Wilaya ya Hai kuna vikundi kama hivyo eneo la mkondo maji wa Hai West 63 na Wilaya ya Mwanga inafanya kazi na vikundi vya mkondo maji wa Mto Mala 57.

Kadhalika, alisema katika Wilaya ya Moshi, Floresta Tanzania inafanya kazi na vikundi vya mkondo maji wa Mto Ghona 95, huku Wilaya ya Rombo ikifanya kazi na vikundi 48 na Wilaya ya Same, ambako wanafanya kazi na vikundi 313 katika mkondo maji wa Shengena Magharibi, Shengena Mashariki vikundi 67 na Mto .Saseni, ambao una vikundi 114.

**Kadhalika, alisema katika Wilaya ya Moshi, Floresta Tanzania inafanya kazi na vikundi vya mkondo maji wa Mto Ghona 95, huku Wilaya ya Rombo ikifanya kazi na vikundi 48 na Wilaya ya Same, ambako wa-**

Mkurugenzi wa Shirika la Floresta Tanzania, Richard Mhina, alisema mradi huo unalenga kuwafikia watu 5,000 kutoka Mkoa wa Kilimanjaro, ambapo asilimia 60 ni vijana na asilimia 40 ni watu wazima.

Aidha, alisema mradi huo siyo tu unalenga kuongeza uwezo wa kiuchumi wa makundi hayo, bali pia kuwezesha vijana na wanawake kuwa wahamasishaji wakuu wa sekta ya kilimo na maendeleo ya kijamii.

Mhina, alisema mradi huo unalenga kuwafikia watu 5,000 kutoka Mkoa wa Kilimanjaro, ambapo asilimia 60 ni vijana na asilimia 40 ni watu wazima.

Aidha, alisema mradi huo siyo tu unalenga kuongeza uwezo wa kiuchumi wa makundi hayo, bali pia kuwezesha vijana na wanawake kuwa wahamasishaji wakuu wa sekta ya kilimo na maendeleo ya kijamii.

Zaidi Mhina alisisitiza: "Mradi huu pia unasaidia kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi na kupanda kwa bei za vyakula, mafuta na mbolea kutokana na changamoto za kimataifa kama vile uvamizi wa Urusi na Ukraine."

Maonyesho hayo ya mbegu yalitanguliwa na kauli mbiu isemayo, 'mbegu zetu, maisha yetu, panda leo kwa kesho endelevu'.

# BBT yatengewa mil.600/- kuongeza thamani mkonge

**Na Hamida Kamchalla,** TANGA

WAZIRI wa Kilimo, Hussein Bashe, amesema serikali imekitengea Kituo Atamizi cha Mkonge (BBT) kilichoko mkoani Tanga, Sh. milioni 600 kwa ajili ya kukifanya kuwa kongani ndogo ya kuongeza thamani mkonge na mazao mengine madogo ya viungo.

Alisema hayo mwishoni mwa wiki mkoani Tanga wakati akizindua kituo hicho.

Bashe alisema serikali imeweka dhamira ya kukamilisha ombi la Bodi ya Mkonge Tanzania (SBT), kwa pande zote mbili za muungano, yaani upande wa Tanga (Bara) na Visiwa vya Zanzibar.

"Kituo hiki na kwa mkoa huu wa Tanga, hapa patageuka kongano dogo, ambalo litawekwa vifaa vyote vidogo vidogo vya kuongeza thamani mkonge na mazao mengine ya kilimo.

"Hivyo, fedha hii iliyotengwa na serikali itakwenda kununulia vifaa na malighafi vitakavyosaidia wajasiriamali kutengeneza bidhaa zao," alisema Bashe na kuongeza:

...Baada ya kuchukua mikopo yao, kina mama na vijana watakuwa wanakuja hapa na kila anayetaka kutengeneza bidhaa yake malighafi zote watazikuta hapa. Kwa hiyo, watatumia kama sehemu ya kuzalishia mali na kwenda kuuza kwenye biashara zenu."

# Samia apiga simu kuwapongeza walimu matumizi nishati safi

**Na Gwamaka Alipipi**

RAIS Samia Suluhu Hassan amewapongeza walimu mkoani Arusha kwa kuunga mkono matumizi ya nishati safi ya kupikia, huku akiwaahidi kuwapatia majiko ya gesi.

Alitoa pongezi hizo juzi baada ya kupiga simu wakati wa maadhimisho ya Siku ya Walimu Duniani, iliyoenda sambamba na ugawaji mitungi ya gesi na majiko kwa walimu yaliyotolewa na Oryx gas, kuratibiwa na Mbunge wa Arusha Mjini, Mrisho Gambo.

Rais Samia alisema: "Nimepiga simu niwapongeze walimu, leo mna mkutano wa nishati safi ya kupikia kwa hiyo ninawapongeza kwa kuibeba hiyo agenda. Niwaahidi tu mchango wangu katika hilo ndugu walimu katika majiko yatakayotoka mimi nitakuja kujazia baadaye".

Kadhalika aliwaeleza walimu hao kwamba changamoto zinazowakabili anazifahamu, kwamba serikali inaendelea kuzifanyia kazi.

Kwa upande wake Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Omar Kipanga aliyemwakilisha Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Profesa Adolf Mkenda alimshukuru Rais Samia kwa jitihada anazofanya za kuendelea kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia.

"Katika siku hii ya leo ya kuadhimisha siku ya walimu kauli mbiu yetu inahusu masuala ya nishati safi ya kupikia na kama mnavyofahamu Rais DK. Samia Suluhu Hassan amezungumza na sisi leo lakini tunakumbuka Mei mwaka huu alizindua kampeni hii ya utumiaji wa nishati safi ya kupikia na malengo yetu kama serikali ni kuhakikisha itakapofika mwaka 2034 asilimia 80 ya Watanzania wawe wamefikiwa katika matumizi ya nishati safi ya kupikia," alisema.

Katika sherehe hiyo, Oryx Gas Tanzania kwa ushirikiano na wadau mbalimbali walitoa mitungi ya gesi 5,000 yenye thamani ya Sh. milioni 417.5 kwa walimu wa shule za msingi na sekondari jijini Arusha.

Alisema Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia wamelibeba jambo hilo na wameanza na taasisi za elimu ambazo zinahudumia watu zaidi ya 100 kuanza kutumia nishati safi ya kupikia.

Mkurugenzi Mkuu wa Oryx Gas Tanzania, Benoit Araman, alisema kwa kushirikiana na Mbunge wa Arusha Mjini wamewapatia walimu majiko na mitungi ya gesi.

"Naomba niwagusie walimu na maprofesa sito tu kwa sababu tunasherehekea leo Siku ya Walimu Dunuani bali naamini ninyi nyote ni kiungo muhimu kwa jamii na taifa letu. Hivyo natoa ombi maalum kwa walimu kuwa mabalozi wa nishati safi ya kupikia." alisema.

Mbunge wa Arusha Mjini, Mrisho Gambo alisema anatambua mchango wa walimu na katika kusherehekea Siku ya Walimu Duniani amelazimika kuwapa zawadi hiyo kwa kila mwalimu ili wakawe mabalozi wa nishati safi.





# Bil.100/- zapeleka umeme kwa wachimbaji wadogo

**Na Alphonse Kabilondo,** GEITA

NAIBU Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Dotto Biteko amesema serikali imetenga Sh.bilioni 118 kwa ajili ya kupeleka umeme kwenye maeneo ya wachimbaji wadogo nchini. Amesema katika fedha hizo, Mkoa wa Geita umetengewa Sh. bilioni Saba.

Dk. Biteko alitoa kauli hiyo juzi mkoani Geita wakati akizindua Maonesho ya Saba ya Kitaifa ya Teknolojia ya Madini yaliyofanyika katika viwanja vya EPZA bomba mbili.

Alisema hatua hiyo itasaidia kuondoa adha ya wachimbaji wadogo kutumia gharama kubwa kuendesha mitambo na shughuli zao zinazohitaji umeme kwa kutumia majenereta. Aidha, aliwataka wachimbaji na wafanyabiashara wa madini kushirikiana vyema na serikali kwa kuiuzia Benki Kuu ya Tanzania (BoT) asilimia 20 ya madini kabla ya kuyauza na kuyasafirisha kwenda nje.

Katika hatua nyingine, Dk.Biteko aliridhishwa na huduma zinazotolewa na Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), kwa kuwafikia wafanyabiashara na wachimbaji kwa kutoa huduma na hamasa ya kurasimisha biashara zao.

Naye, Waziri wa Madini Anthony Mavunde alisema katika kuboresha sekta ya madini serikali imeongeza bajeti yake kutoka Sh. bilioni 90 hadi kufikia Sh.bilioni 231 kwa mwaka 2024|25 ambapo bajeti hiyo imeelekezwa katika ununuzi wa helkopita, ujenzi wa maabara mbili ambayo moja itajengwa mkoani Geita.

**Aidha, alipiga marufu raia wa kigeni kuweka uchimbaji katika migodi yenye leseni ya uchimbaji mdogo na kuwa hali hiyo imekuwa ikisababisha migogoro ya mara ..**

Aidha, alipiga marufu raia wa kigeni kuwekeza uchimbaji katika migodi yenye leseni ya uchimbaji mdogo na kuwa hali hiyo imekuwa ikisababisha migogoro ya mara kwa mara.

Mkuu wa Mkoa wa Geita, Martine Shigela alisema kwa kipindi cha miaka mitatu leseni 316 zimetolewa kwa wachimbaji mkoani humo.

Alisema kuwa kati ya leseni hizo 30 zimetolewa kwa wanawake, huku wachimbaji wadogo wakizalisha zaidi kilo 16,000 za madini na kulipa kodi ya serikali zaidi ya Sh.bilioni 165.

Alisema maadhimisho hayo kwa mwaka jana yalikuwa na washiriki 350 kutoka mikoa mbalimbali na wengine kutoka nje ya Tanzania na kuwa mwaka huu wameshiriki zaidi ya 800.

Rais wa Shirikisho la Vyama vya Wachimbaji wa Madini nchini (FEMATA), John Bina, alisema wamekubaliana wachimbaji na wanunuzi kuiuzia BoT asilimia 20 ya madini wanayopata kabla ya kuuza na kuyasafirisha.

Ofisa Leseni Mwandamizi kutoka BRELA, Koyan Aboubakar alisema dira ya wakala huo kwa sasa ni kuwafikia wadau wengi zaidi pamoja na kutoa huduma za papo kwa papo.



Mkuu wa Mkoa wa Geita, Martine Shigella (kulia), akimkabidhi Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Said Mtanda, Mwenge wa Uhuru jana, ukitarajiwa kuzungushwa zaidi ya kilomita 649 mkoani humo na kuzimwa Oktoba 14, 2024 na Rais Samia Suluhu Hassan katika Uwanja wa CCM Kirumba. **PICHA: VITUS AUDAX.**

# Wafanyabiashara walia kukithiri mikopo umiza

**Na Rose Jacob,** MWANZA

WAFANYABIASHARA mkoani Mwanza wamesema kinachowakwamisha kuendelea kiuchumi, kukuza biashara zao ni kukithiri kwa mikopo yenye riba kubwa 'mikopo umiza'.

Wamesema mikopo hiyo huwafanya kushindwa kutekeleza vyema kazi zao hali inayowafanya wengi wao kufilisika na kuwa maskini.

Walisema hayo juzi wakati wakizungumza na viongozi na maofisa wa benki ya Ecobank waliofika jijini hapa kutoa mafunzo ya kuendesha biashara, kukuza mitaji kwa wanawake na wafanyabiashara.

Mmoja wa wafanyabiashara hao, Lemison Owiso alisema ukubwa wa riba katika mikopo wanayokopa kupitia benki mbalimbali au kampuni zinazojihusisha na utoaji wa mikopo inasababisha wengi wao kufilisika.

Mkuu wa kitengo cha biashara wa benki hiyo, Joyce Ndyetabura alisema: "Wanawake wamekuwa wakiogopa kufanya biashara kubwa kwa sababu ya kukosa mitaji, wanaogopa kwenda kwenye benki kwa sababu hawana cha kuweka kama dhamana, sisi tunatoa mtaji kwa mwanamke yeyote ambaye anamradi uliyoanza kazi au tenda kwenye kampuni yoyote iwe binafsi au ya kiserikali, kikubwa iwe imesajiliwa kisheria."

# RC asisitiza faragha ya kujisitiri hedhi kwa wanafunzi

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MKUU wa Mkoa wa Shinyanga, Anamringi Macha, amesema wanafunzi wa kike wanahitaji faragha ya kujisitiri hedhi wanapokuwa katika mazingira ya shule, ili kulinda utu wao.

Alisema hayo juzi Taasisi ya Flaviana Matata Foundation ikikabidhi choo cha kisasa chenye matundu 12, kwa ajili ya wanafunzi wa kike katika Shule ya Sekondari Masekelo iliyopo katika Manispaa ya Shinyanga, kikiwa na chumba maalum cha kujisitiri hedhi.

Alisema suala la kujisitiri hedhi linahitaji faragha na hivyo kuipongeza taasisi hiyo kwa hatua hiyo muhimu iliyoweka alama kwa wanafunzi shuleni hapo.

"Mwanafunzi wa kike anahitaji faragha kujisitiri hedhi na huo ndiyo utamaduni na heshima ya binadamu na kulinda utu wao," alisema Macha.

Alisema chumba maalum cha kujisitiri hedhi ni muhimu sana shuleni, kwamba licha ya kulinda faragha, pia itaongeza ufaulu mzuri kwa wanafunzi wa kike, sababu hawatakosa vipindi vya masomo darasani.

Mjumbe wa Bodi kutoka Flaviana Matata Foundation, Wilhemina Malima, alisema chumba maalumu cha kujisitiri hedhi ni muhimu kwa wanafunzi shuleni katika kukuza taaluma zao kwa sababu kwa mwezi wanakosa siku tano za masomo, ambapo kwa mwaka mzima hukosa siku zaidi ya 50.

Mratibu wa Mfuko wa Ruzuku kwa Wanawake Tanzania (WFT-Trust) mkoani Shinyanga, Glory Mbia, alisema miundombinu ya choo hicho inapaswa kutunzwa pamoja na kufanyiwa usafi wa mara kwa mara.

Mkurugenzi Mtendaji taasisi hiyo, Flaviana Matata, alisema wamekuwa wakiunga mkono sekta ya elimu hususani kwa wanafunzi wa kike. Alisema katika mkoa huu wamekuwa na mradi wa ujenzi wa vyoo vya aina hiyo katika baadhi ya shule.

Flaviana alisema katika shule hiyo wamejenga choo cha wasichana chenye matundu 12 kikiwa na chumba maalumu cha kujisitiri hedhi pamoja na kichomea taka na wanawafadhili wanafunzi watoto kimasomo.

Alisema kila mwezi wanawapatia wasichana 30 taulo za kike katika shule hiyo.

Mkuu wa Shule ya Sekondari Masekelo, Vicent Kanyogota, alisema upatikaji wa chumba maalumu cha kujisitiri hedhi shuleni hapo kutasaidia kupunguza utoro kwa wanafunzi wa kike na hata kufanya vizuri kitaaluma.

# Nipashe Spotika



UJUE UTAMADUNI WA KUBADILISHANA JEZI UK. 12-13



# TEN HAG NA KUTI KAVU MAN UNITED

**MANCHESTER,** England

ZILIPOTIMIA dakika 90 kule kwenye Uwanja wa Dragao, kocha Erik ten Hag alionekana kukaribia mwisho wake.

Timu yake ya Manchester United ilikuwa imepoteza uongozi wa mabao mawili kwa moja dhidi ya Porto na ilikuwa ikielekea kupoteza.

Kichapo ambacho huenda hakikuthibitisha mwisho wa muda wa Ten Hag ndani ya Old Trafford lakini bila shaka kingemwacha akitetemeka, zaidi ya hapo awali.

Lakini kabla hali hiyo kutimia, Harry Maguire aliruka kwa kichwa na kusawazisha na kupunguza shinikizo kwa kocha wake.

"Tutafika tunakoelekea," alisema Ten Hag akiiambia TNT Sports. "Usituhukumu kwa wakati huu, tuhukumu mwishoni mwa msimu.

"Tupo kwenye mchakato, tutaboresha. Tumekuwa na misimu miwili ambayo tumefika fainali, tutaendelea na kupambana."

Huku United kwa sasa ikiwa katika nafasi ya 14 kwenye jedwali la Ligi Kuu England (kabla ya mechi za jana), na uvumi kutokana na kichapo cha mabao 3-0 kutoka kwa Tottenham Hotspur, kwamba Ten Hag alikuwa na mechi mbili kuokoa kibarua chake, uamuzi wa Mholanzi huyo kufungasha virago huenda ukafika mapema zaidi ikiwa hakutakuwa na maboresho makubwa.

"Unaweza kuona uhusiano kati ya wafanyakazi na timu," aliongeza Ten Hag.

"Wachezaji wapo pamoja, wana ari kubwa na wanataka kuyafikia malengo yao, tuna mawazo mazuri, lakini katika sehemu za ulinzi lazima tuongeze nguvu.

"Tulicheza mechi kadhaa bila kufungwa ikimaanisha tunaweza kuimarisha safu ya ulinzi, kwa hivyo lazima turudi kwenye tabia hiyo."

### TAKWIMU

Licha ya Ten Hag kuendelea kujiamini yeye na timu yake, takwimu zinaonesha kwamba ukosoaji kutoka nje huenda upo sahihi.

Tangu Mholanzi huyo ajiunge na klabu hiyo mwaka 2022, hakuna klabu yoyote ya Ligi Kuu iliyofungwa mabao matatu au zaidi katika mechi mara nyingi zaidi katika michuano yote kuliko mabao 24 ya United.

Zaidi ya hayo, katika mechi 62 walizocheza tangu kuanza kwa msimu uliopita, United wamefungwa mara 31 - ikiwa ni zaidi ya timu yoyote ya sasa ya Ligi Kuu England.

Wamecheza mechi nne bila kufungwa kufikia sasa msimu huu lakini kwa timu yenye matamanio ya kuwania mataji makuu nyumbani na Ulaya, kuruhusu kufungwa mabao mawili au zaidi katika kila mechi ni jambo lisilopendeza.

Ina maana kwamba licha ya kufanikiwa kufunga mabao matatu katika mechi nne zilizopita za ugenini za Ulaya, United wamepoteza mechi mbili na hawajashinda hata moja.

Sare ya huko Porto pia ilikuwa mfano mwingine wa tabia isiyohitajika ambayo wameanzisha ya kutupa uongozi.

'Mashetani Wekundu' hao sasa wamecheza mechi tano bila ushindi katika mashindano ya Ulaya licha ya kuongoza kwa angalau mabao mawili kati ya matatu kati ya hayo.

United sasa wamecheza mechi tano bila ushindi katika mashindano ya Ulaya licha ya kuongoza kwa magoli mawili katika mechi tatu.

Kwa kuwa tayari wamekabiliwa na maswali juu ya uwezo wao wa kufunga mabao msimu huu, kwa kweli haiashirii vema kwamba wanaweza kuruhusu mabao kama haya - na hata wanapojiweka mbele, wanawaruhusu wapinzani wao kukomboa.

### HATIMA YAKE

Hata baada ya kuepuka kushindwa nchini Ureno, Ten Hag bado anatazamwa na jicho la karibu kabla ya mechi ya jana Jumapili ya Ligi Kuu dhidi ya Aston Villa.

Alisalia katika klabu hiyo msimu huu, baada ya timu yake kumaliza katika nafasi ya nane na kushinda Kombe la FA.

Ingawa matokeo mabaya ya msimu huu yameshuhudia shinikizo kwa kocha huyo mwenye umri wa miaka 54 kuongezeka tena, Mark Ogden, mwandishi mkuu wa ESPN, hatarajii kwamba Ten Hag atatimuliwa hata iwapo United itapoteza katika Uwanja wa Villa Park.

"Nitashangaa ikiwa atapoteza kazi yake," aliiambia BBC Radio 5 Live.

"Manchester United wanatumaini ataboresha mambo. Ni wazi anapitia shinikizo kubwa"

Lakini ni muda gani atasalia ikiwa matokeo hayataboreka pia ni suala lingine.

"Tabia ya wachezaji ni kama wamehudhuria somo la hisabati na mwalimu ambaye hawapendi na wote wanatoka wakiwa wamechanganyikiwa," anaongeza Ogden.

"Kwa kweli hakuna aina yoyote ya uchangamfu kutoka kwa Erik ten Hag hadi kwa wachezaji. Ten Hag hana haiba ya kusimamia klabu kubwa."

## ISIKUPITE

BAO alilofunga Bukayo Saka wakati Arsenal ikishinda 3-1 dhidi ya Southampton juzi, linamfanya winga huyo kuhusika katika mabao 10 kwenye mashindano yote msimu huu akiwa amefunga matatu na kutoa pasi za mwisho 'assists' saba hadi sasa.



# UJUE UTAMADUNI WA KUBADILISHANA JEZI



Lionel Messi na Kipa wa Ecuador, Hernan Galindez, wakibadilishana jezi baada ya mechi ya kuwania kufuzu Kombe la Dunia 2024 dhidi ya Argentina Septemba 8, 2023. Argentina ilishinda bao 1-0. **PICHA: MTANDAO**

**LONDON,** England

WAKATI mlinzi wa Inter Milan, Francesco Acerbi alipomwomba nyota wa Manchester City, Erling Haaland, kwa utani jezi mbili baada ya mechi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, huenda alikuwa akijaribu bahati yake.

**Kubadilishana jezi kwa muda mrefu umekuwa utamaduni katika soka, hata hivyo, na wachezaji wengi wanaona fahari kubwa katika makusanyo ya kuvutia wanayoweza kuweka majumbani mwao.**

Baadhi ya jezi huwa zinahitajika zaidi kuliko zingine, huku timu moja ikisafiri kwenda kwenye mechi ikiwa na mifuko kadhaa iliyojaa jezi zake ili kuzitoa kwa niaba ya mchezaji wao nyota.

Lakini wachezaji hufanya nini hasa na jezi wanazozipata? Na je, jezi hizo hutendewa usawa mara tu ubadilishanaji unapofanywa mbele ya kamera?

### JEZI NYINGI

Wachezaji wengi wameonesha mkusanyiko wao wa jezi za soka kwenye mitandao ya kijamii, huku wakitenga chumba kwa ajili ya kuonesha jezi zinazoheshimika zaidi.

Lionel Messi, ambaye si mgeni katika mahitaji ya kubadilishana jezi ambaye ni mchezaji bora zaidi wa wakati wote, alichapisha picha ya mkusanyiko wa jezi zake ambao ameziweka ukutani.

Beki wa zamani wa Barcelona, Gerard Pique anasema alikuwa akikagua chumbani mwake alipokutana na jezi za wachezaji wengi ambao unajumuisha jezi za Messi, Andrea Pirlo na David Beckham.

Pique aliongeza kuwa alikuwa ameitengenezea fremu jezi alizobadilishana baada ya fainali ya Kombe la Dunia 2010, ambapo timu yake ya Hispania iliifunga Uholanzi, kutoka kwa mshambuliaji, Klaas-Jan Huntelaar.

Lakini mkusanyiko wa tuzo uliovutia zaidi kati ya yote kwa hakika unakwenda kwa kocha wa Italia, Luciano Spalletti.

Baada ya kuiongoza Inter Milan kurudi kwenye mashindano ya Ulaya mwaka 2019, Spalletti alijumuishwa katika mkusanyiko wa "majina kutoka Ligi ya Mabingwa", ya wababe wengi wa mchezo huo.

### JEZI MUHIMU

Wachezaji wengine lazima washughulikie mahitaji makubwa zaidi ya jezi zao kuliko wengine.

Messi anajua hili kama mtu yeyote, lakini nyota huyo wa Argentina ameunda mifumo ya kukabiliana na tatizo hilo. Golikipa Kipa Emiliano Martinez aliiambia Prime Sport kwamba mchezaji huyo wa Timu ya Taifa ya Argentina, hutayarisha jezi 650 za Messi kwa kila mechi mbili, zitakazogawanywa kati ya wachezaji, wafanyakazi, wafadhili na hata wasimamizi karibu na siku za mechi.

Martinez mara kwa mara huombwa jezi za Messi na, kwenye Kombe la Dunia la 2022, alipunguza pigo la kushindwa kwa Poland na Argentina kwa mchezaji mwenzake wa Aston Villa, Matty Cash kwa kumpa moja.

Lakini si majina makubwa tu, Wayne Rooney alikiri kwamba kiburi chake wakati akicheza kilimaanisha kwamba hatawahi kuomba jezi kwa mpinzani; hata hivyo, daima angemheshimu mchezaji yeyote ambaye angeomba jezi yake.

Na kwa hivyo, ingawa hana jezi za wachezaji kama vile Zinedine Zidane, nyota huyo wa zamani wa England na Manchester United anamiliki jezi ya Andorra kutoka kwa Ildefons Lima - ambaye alifurahi kugundua Rooney alikuwa ameiweka.

"Siku zote nilimheshimu mchezaji yeyote aliyekuja na kuniomba jezi yangu," anasema Rooney akiiambia BBC Sport.

"Nimeona wachezaji ambao wanaitupa tu kwenye mkusanyiko wa jezi walionao na hawapendezwi, ambapo mara zote mimi huonesha heshima na kuipeleka nyumbani ili kuihifadhi."

### UTAMADUNI ULIKOANZIA

Utamaduni wa kubadilishana jezi unasemekana ulianza nchini Ufaransa, baada ya kuishinda England, ilipoomba kubadilishana na wapinzani wao ili iwe kukumbuka ya ushindi wao wa mwaka 1931.

Mojawapo ya mazungumzo mashuhuri katika historia yalifanyika mnamo 1970, wakati nyota wa Brazil, Pele na nyota wa England, Bobby Moore walipobadilishana jezi baada ya mechi ya makundi ya Kombe la Dunia kati ya mataifa hayo mawili nchini Mexico.

Mkusanyiko wa jezi siku hizi ni chanzo cha kupendeza na faraja kwa wengi.

Lakini kitu ambacho hakijaonekana katika miaka ya hivi karibuni ni kubadilishana kwa jezi wakati wa muda wa mapumziko.




### WALIKERA

Mario Balotelli alionywa na Liverpool baada ya kubadilishana jezi na Pepe wa Real Madrid wakati timu yake ilipokuwa nyuma kwa mabao 3-0 wakiwa wanaelekea mapumziko mwaka 2014.

Na mwaka 2016 Eden Hazard alizomewa na mashabiki wa Chelsea kwa kubadilishana jezi na winga wa Paris St-Germain, Angel di Maria.

Wakati wa kampeni za Ligi ya Mabingwa mwaka jana, Haaland aliombwa wabadilishane jezi wakati wa mapumziko na nahodha wa Young Boys, Mohamed Ali Camara, baada ya kupoteza 3-0.

Kocha wa zamani wa Manchester United, Alex Ferguson pia hakufurahishwa na mshambuliaji, Ruud van Nistelrooy aliporejea kwenye chumba cha kubadilishia nguo akiwa na jezi ya Manchester City baada ya timu hiyo kupoteza kwa mabao 3-1.

Kiungo wa kati wa zamani wa England, Steve Hodge alijipatia pauni milioni 7.14 baada ya kuuza jezi ya Diego Maradona 'Hand of God' katika robo fainali ya Kombe la Dunia mwaka 1986 katika mnada wa mwaka 2022.

Wakati huo huo, jezi inayosemekana kuwa ya Phil Foden kutoka Timu ya Taifa ya England katika robo fainali ya Euro 2020 dhidi ya Ukraine, aliyopewa kipa Georgiy Bushchan, iliorodheshwa hivi majuzi kwenye mtandao wa eBay kwa pauni 2,999.

Mshambuliaji wa zamani wa Ligi Kuu ya England, Chris Sutton alisema kuhusu mkusanyiko wa jezi zake: "Watoto wangu wana baadhi yazo, lakini nina jezi ninayoipenda zaidi, ambayo ni ya Henrik Larsson aliporudi Celtic akiwa na Barcelona.

"Sijawahi kupenda kubadilishana jezi kama tungepoteza. Sikuwa mmoja wa wachezaji ambao wangemwomba mtu jezi wakati wa mapumziko.

"Kwa hiyo sikujisumbua sana kufanya hivyo, ingawa nimebadilisha mtazamo wangu sasa nimeacha kucheza.

"Ningetamani ningekuja zaidi kuhusu kufanya hivyo baada ya kuona jinsi Steve Hodge alivyovaa jezi ya Diego Maradona, lakini kuwa makini, ni mambo mazuri kuwa nayo unapoangalia nyuma kwenye kazi yako."

## Nukuu

"Huu ni msimu wangu wa sita sasa na ninajua unahusu nini, ninajua kuwa unapitia nyakati ngumu na kila kitu, kila mtu anakurundikia juu yako, lakini kama mwanasoka, ni rahisi kuangalia huku na kule na kulaumu wachezaji wenzako, au kulaumu wafanyakazi au mbinu, ni lazima ujiangalie. Lazima uchukue jukumu na kila mmoja wetu anapaswa kufanya vizuri zaidi katika nyakati hizi," **Beki wa Manchester United, Harry Maguire**



"Sidhani kama tunaweza kushindana na Man City au Arsenal, sifikirii hivyo, hatuko tayari. Sababu ni kwamba City imefanya kazi na kocha mmoja kwa miaka tisa na Arsenal kwa miaka mitano. Ikiwa unataka kushindana kwa mambo makubwa unahitaji wakati huo. Fikiria sisi, miezi mitatu ... hivyo ni tofauti kubwa, hatuwezi kushindana na klabu hizo," **Kocha wa Chelsea, Enzo Maresca, baada ya kuifunga Gent mabao 4-2 kwenye Ligi ya Europa.**



"Ana uwezo wa kubadilika na kuamua michezo. Huo ni ukomavu wake na ni hatua nyingine katika kile anachotaka, unapofanya hivyo nyumbani, kwenye michezo mikubwa na timu inapomhitaji, hiyo ndiyo inafafanua mchezaji wa kiwango cha juu. Ikiwa tunataka kuwa kileleni, wakati mwingine wachezaji wanapaswa kuunda nyakati hizo na hakika alifanya hivyo tena leo [juzi]," **Kocha wa Arsenal, Mikel Arteta, akimzungumzia winga wa timu hiyo, Bukayo Saka**






Kiungo mshambuliaji wa Yanga, Pacome Zouzoua, akitafuta mbinu za kumtoka beki wa Pamba Jiji, Pauline Kasindi, katika mchezo wa raundi ya saba ya Ligi Kuu, uliochezwa Alhamisi iliyopita kwenye Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam. Yanga ambayo ndiyo timu pekee Ligi Kuu Tanzania Bara iliyoshinda mechi zote ilizocheza na kutoruhusu wavu wake kuguswa, ilishinda mabao 4-0.

# REKODI KUMI KALI ZA RAUNDI YA SABA LIGI KUU

**Na Adam Fungamwango**

LIGI ya soka Tanzania Bara imeingia kwenye raundi ya saba, timu nyingi zikiwa zimefikisha michezo hiyo, zingine zikibaki na viporo kwa baadhi ya mechi za raundi za nyuma kutokana na sababu mbalimbali, ikiwamo kushiriki michezo ya kimataifa, hususan, Simba, Yanga, huku Azam na Coastal Union zikiwa zimeshamaliza viporo vyao baada ya kuaga kimataifa.

**Ligi hiyo imesimama kwa wiki mbili kupisha Kalenda ya Shirikisho la Mpira wa Miguu Duniani (FIFA), ambapo baadhi ya wachezaji watakwenda kuunda vikosi vya timu zao za taifa.**

Baadhi ya wachezaji wa Tanzania wamekwenda kwenye kambi ya Timu ya Taifa ya Taifa Stars kwa ajili ya kujiandaa na mechi dhidi ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, kusaka tiketi ya kufuzu fainali za Mataifa ya Afrika (AFCON) 2025, zitakazofanyika nchini Morocco.

Wakati ligi imesimama, mechi nyingi za raundi ya saba zilizomalizika wiki hii zimeweka rekodi kadhaa kwa timu mbalimbali.

Katika makala haya tunakuletea rekodi hizo na zingine zilizowekwa hadi kufikia raundi hiyo, twende sasa...

### 1# Yanga ushindi asilimia 100

Yanga hadi kufikia raundi ya saba ndiyo timu pekee ambayo imeshinda michezo yote iliyocheza na kutoruhusu wavu wake kuguswa. Ushindi wa mabao 4-0 iliyoupata Alhamisi iliyopita dhidi ya Pamba Jiji FC, kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam, umeifanya kushinda michezo yote minne mfululizo.

Mbali na hilo, Yanga ndiyo timu pekee mpaka sasa haijaruhusu wavu wake kuguswa kwenye Ligi Kuu msimu huu, ikicheza mechi nne, kushinda zote, imefunga mabao manane, haijaruhusu bao, ikishika nafasi ya nne kwenye msimamo wa Ligi Kuu.

### 2# Simba imefunga mengi nyumbani

Simba ndiyo timu iliyofunga mabao mengi ikicheza kwenye uwanja wake wa nyumbani hadi kufikia raundi hiyo. Sare ya mabao 2-2 nyumbani, Ijumaa iliyopita dhidi ya Coastal Union, Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam, imeifanya kufikisha mabao tisa ya kufunga kwa michezo mitatu tu iliyocheza.

Imeyapata kwa kuifunga Tabora United mabao 3-0, Fountain Gate 4-0 na sare ya Ijumaa zote zikichezwa kwenye uwanja huo uliopo, Mwenge Dar es Salaam, na kuzipiga kumbo timu zote za Ligi Kuu.

### 3# Namungo haijapata sare

Namungo ndiyo timu pekee ambayo mpaka sasa haijapata sare yoyote kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara hadi kufikia raundi ya saba. Timu hiyo ambayo imecheza michezo sita, ikiwa na kiporo kimoja, imeshinda michezo miwili na kupoteza minne.

Hadi ligi inakwenda mapumzikoni, inakamata nafasi ya 12 kwenye msimamo ikiwa nafasi ya sita.

### 4# Fountain Gate mabao mengi ugenini

Timu ya Fountain Gate imefunga mabao mengi ikicheza ugenini kuliko nyingine yoyote kwenye Ligi Kuu mpaka sasa. Imefunga mabao saba ikicheza nje ya uwanja wake wa nyumbani, idadi ambayo haijafikiwa na timu yoyote.

### 5# JKT Tanzania, Mashujaa zafungwa

Michezo ya raundi ya saba ya Ligi Kuu, imeshuhudia timu za Mashujaa FC na JKT Tanzania zikipoteza mechi zao kwa mara ya kwanza.

Baada ya kucheza michezo mitano, ikishinda miwili na sare tatu, Mashujaa ilipata kipigo cha kwanza tangu kuanza kwa ligi dhidi ya KenGold kwa bao 1-0, mechi iliyochezwa, Ijumaa iliyopita, Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya.

JKT Tanzania ambayo ilicheza pia michezo mitano ilipata kipigo kwenye mechi ya sita, ilipolala bao 1-0 nyumbani, Uwanja wa Lake Tanganyika, Kigoma dhidi ya Singida Black Stars.

Timu zote mbili zimepoteza michezo yao zilipocheza mechi zao za sita, lakini zikiwa raundi ya saba.

### 6# Pamba Jiji haijui utamu wa ligi

Pamba Jiji ndiyo timu pekee kwenye Ligi Kuu ambayo haijaonja ushinda mechi yoyote mpaka sasa.

Licha ya kucheza michezo saba kwenye Ligi Kuu, haijaonja utamu wa ligi, ikicheza kwa mara ya kwanza baada ya miaka 22. Timu hiyo inayoburuza mkia, imetoa sare mechi nne, kupoteza mitatu.

### 7# KenGold, Prisons zaona mwezi

Hatimaye timu za Kengold na Prisons zote za Mbeya, zimeshinda michezo yake ya kwanza kwenye raundi ya saba ya Ligi Kuu.

KenGold, ambayo ilicheza mechi zake sita za kwanza, ikiwa ni mara yake ya kwanza Ligi Kuu bila kupata ushindi wowote, hatimaye ilipata ushindi, Ijumaa iliyopita, Uwanja wa Sokoine, Mbeya, ilipoichapa JKT Tanzania bao 1-0. Kabla ya hapo ilikuwa imepoteza mechi tano mfululizo za kwanza, kabla ya kutoka sare moja, na baada ya hapo ikapata ushindi.

Prisons, baada ya sare nne mfululizo, kabla ya kupoteza moja, hatimaye ilipata ushindi wake wa kwanza, Jumanne iliyopita wa mabao 3-2 dhidi ya Fountain Gate, mechi iliyochezwa, Uwanja wa Sokoine, Mbeya.

### 8# Singida BS ugenini kama nyumbani

Singida Black Stars ndiyo timu iliyozoa pointi nyingi ikicheza viwanja vya ugenini hadi kufikia raundi ya saba.

Timu hiyo ambayo imecheza michezo sita, imeshinda mechi zote nne ilizocheza ugenini, ikikusanya pointi 12, huku ikicheza mechi mbili tu nyumbani, ambazo imeshinda moja na kutoa sare moja, ikipata pointi nne. Inaongoza ligi ikiwa na pointi 16 mpaka sasa.

### 9# Simba sare ya kwanza, yaruhusu mabao

Sare ya mabao 2-2 iliyoipata Simba, Ijumaa iliyopita, Uwanja wa KMC Complex, imeifanya timu hiyo kupata sare ya kwanza kwenye Ligi Kuu baada ya kushinda michezo minne ya kwanza.

Pia imeruhusu wavu wake kuguswa mara ya kwanza, kwani kabla ya mchezo huo, ilikuwa haijaruhusu bao. Inashika nafasi ya pili kwenye msimamo wa Ligi Kuu, ikiwa na pointi 13, sawa na Fountain Gate, lakini ina tofauti nzuri ya mabao ya kufunga na kufungwa.

### 10# Fountain Gate, fowadi wembe, beki njia

Fountain Gate ndiyo timu pekee iliyofunga mabao mengi kwenye Ligi Kuu kuliko timu nyingine yoyote.

Imeshapachika mabao 14 mpaka sasa. Hata hivyo, ndiyo timu iliyoruhusu mabao mengi zaidi wavuni kwake. Imesharuhusu mabao 12 mpaka sasa na inakamata nafasi ya tatu kwenye msimamo wa ligi hiyo, ikiwa na pointi 13.

## JE, WAJUA?



KATIKA mechi 62 walizocheza Manchester United kwenye mashindano yote tangu kuanza kwa msimu uliopita, imefungwa mara 31 – ambazo ni zaidi ya timu yoyote ya sasa ya Ligi Kuu England.



# NEEC yatoa bil. 19/- kwa wananchi 11,382

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

BARAZA la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC) limesema katika kipindi cha miezi sita limetoa mikopo ya Sh.bilioni 19.9 kwa wananchi 11,382.

Katibu Mtendaji wa Baraza hilo, Being' Issa, akizungumza jana wakati wa kikao cha kutambulisha Programu ya Imarisha Uchumi na Mama Samia (IMASA) kwa Mkoa wa Singida, alisema wananchi hao walinufaika na mikopo hiyo katika kipindi cha kuanzia Septemba 2023 hadi Machi 2024.

Kikao hicho kiliwashirikisha wakuu wa wilaya, makatibu tawala wa wilaya, waratibu wawezeshaji wananchi kiuchumi, viongozi wa Jukwaa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, maofisa tarafa na wakuu wa idara na vitengo.

Alisema katika kipindi hicho kampuni 1,906 zimesajiliwa, wananchi 8,826 wamepewa ushauri na mafunzo yametolewa kwa wananchi 11,893.

Issa alisema katika kuhakikisha wananchi wanawezeshwa kiuchumi, Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi limetengeneza mwongozo wa kuongoza taasisi zote zinazosimamia miradi ili ziweze kusaidia wananchi kiuchumi.

"Katika suala la ajira tumeweka utaratibu lazima mkandarasi anapotekeleza mradi zinaanishwa ajira za Watanzania wenye ujuzi na zisizo na ujuzi na mambo hayo yanakuwa kwenye mkataba na baraza tunafuatilia kuona utekelezaji," alisema.

Akizungumza kuhusu Programu ya Imarisha Uchumi na Mama Samia (IMASA), alisema itahusisa wanawake, vijana na makundi maalum na itatekelezwa katika mikoa yote 26 ya Tanzania Bara.

"Programu hii itatekelezwa kwa kipindi cha mwaka mmoja kuanzia Julai 2024 hadi Juni 2025 na itahusisha wanufaika 62,000, na NEEC ndio msimamizi mkuu wa programu kwa kushirikiana na ofisi za wakuu wa mikoa, wakuu wa wilaya, wakurugenzi wa halmashauri na wadau wengine," alisema.

Aliongeza kuwa madhumuni ya programu hiyo ni kupata takwimu za wananchi waliopo kwenye maeneo yao na shughuli wanazozifanya ambapo zitatokana na shughuli za kiuchumi zinazoendeshwa kwenye mikoa yote nchini.

Madhumuni mengine ni kupata takwimu za majukwaa ya uwezeshaji wanawake kiuchumi, kupata mahitaji ya kiuchumi kwenye maeneo husika na kutekeleza programu ya kuwawezesha wananchi kwenye mikoa.

# Daktari ataja chanzo watoto kuzaliwa na mtindio wa ubongo

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

UPUNGUFU wa madini ya chuma mwilini, viini lishe, ulevi uliopindukia, matumizi holela ya dawa bila maelekezo ya daktari, kujifungua katika maeneo yasiyo salama zimetajwa kuwa ni miongoni mwa sababu zinazochangia watoto kuzaliwa na mtindio wa ubongo.

Daktari Bingwa wa Watoto katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma, Pendo Chaula alisema hayo wakati wa mahojiano na Nipashe ikiwa ni maadhimisho ya Siku ya Utindio wa Ubongo. Yaliyobeba kauli mbiu isemayo 'Weka alama yako'.

"Huwezi kuwa mjamzito ukawa unakunywa pombe, unatumia dawa ambazo mjamzito hapaswi kutumia hivi ni vitu vinavyoweza kuchangia kuharibu mfumo wa ubongo wa mtoto kwa kuwa anaendelea kukua."

Hivyo, aliwashauri wajawazito kutotumia kilevi cha aina yoyote, sigara wala dawa za kulevya ili kutopata mtoto mwenye tatizo hilo.

"Tunamshauri mjamzito atumie vyakula ambavyo ni lishe bora, mlo kamili hauna gharama sana kama vile kula ugali, wali, matembele, dagaa, kunywa maji na chungwa moja unapata vitu muhimu katika ukuaji wa mtoto tumboni," alisema.

Pia aliwataka wajawazito kama watakuwa na changamoto zozote za kiafya waende kwa wataalamu wa afya kufanyiwa vipimo ili wapewe dawa kulingana na matatizo ambazo hazina madhara kwa mtoto anayekua.

Kadhalika, alisisitiza kinamama kuhudhuria kliniki wakati wa ujauzito na baada ya kujifungua ili wataalamu wa afya wafuatilie maendeleo ya ukuaji wa watoto.

> **"Wanapojifungua tunashauri wajifungulie hospitali ili anapopata uzazi pingamizi ambao wakati mwingine humweka hatarini mtoto kupata tatizo hilo ni rahisi daktari kushauri...."**

"Wanapojifungua tunashauri wajifungulie hospitali ili anapopata uzazi pingamizi ambao wakati mwingine humweka hatarini mtoto kupata tatizo hilo ni rahisi daktari kushauri uamuzi mwingine wa kumwokoa mtoto," alisema.

Pia alisema mtoto anapozaliwa ni muhimu kuhudhuria ipasavyo kliniki kwa kuwa kuna wengine dalili za tatizo hilo huonekana kipindi hicho cha ukuaji kama vile kushindwa kunyonya vizuri, kulala sana na homa ya manjano.

Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu imeweka mikakati ya kukabiliana tatizo hilo kwenye huduma ya afya, elimu, na usaidizi wa jamii.

Miongoni mwa mikakati hiyo ni programu za mafunzo kwa wataalamu wa afya, wakiwamo madaktari, wauguzi na watoa huduma za utengamao, zinazolenga kuboresha utambuzi na udhibiti tatizo hilo.

Pia, uchunguzi wa mapema ambao unaweza kuboresha kwa kiasi kikubwa matokeo kwa watoto wenye mtindio wa ubongo, kampeni na programu zinafanywa ili kuongeza ufahamu kuhusu ugonjwa wa kupooza kwa ubongo, ishara zake na umuhimu wa kushughulikia mapema.

Pamoja na mikakati hiyo, pia serikali inatoa elimu ya kupunguza unyanyapaa kwa kuwaunganisha watoto wenye mtindio wa ubongo katika shule za kawaida ili kuhakikisha wanapata usaidizi unaofaa na malazi.



Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Alhaji Jabir Shekimweri (wa tatu kulia), akishiriki bonanza pamoja viongozi na wananchi wa Jiji la Dodoma lililofanyika Dodoma juzi, la kuhamasisha umma kushiriki mchakato wa uchaguzi wa serikali za mitaa utakaofanyika nchini kote Novemba 27, mwaka huu. **PICHA PETER MKWAVILA**

# Halmashauri yajipanga dhidi ya magonjwa mlipuko

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

HALMASHAURI ya Jiji la Dodoma imewaagiza kampuni na vikundi vya uzoaji taka kuwa na vifaa vinavyojitosheleza kwa ajili ya wafanyakazi wao, ili kuwalinda na milipuko ya magonjwa.

Kaimu Ofisa Mazingira na Udhibiti wa Taka ngumu mkoani Dodoma, Ally Mfinanga aliyasema hayo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu maandalizi ya kuelekea kipindi cha msimu wa mvua ili kuliweka Jiji la Dodoma katika mazingira ya usafi.

Alisema moja ya sehemu kubwa ambayo Jiji la Dodoma linaweza kukabiliana na kuliweka katika hali ya usafi ni pamoja na kampuni na vikundi vya uzoaji taka kuhakikisha wanakuwa na vitendea kazi na vifaa kwa ajili ya wafanyakazi wao.

Alieleza katika kipindi cha mvua baadhi ya maeneo kama vile ya kuhifadhia taka kwenye masoko na kwenye mifereji kumekuwa na tatizo la uzoaji taka. "Hivyo tunapoelekea kipindi cha mvua ninawaagiza kampuni zinazofanya usafi pamoja na vikundi na wadau wa mazingira wahakikishe wanakuwa na vifaa vilivyoboreshwa ili kukabiliana na magonjwa yanayoweza kujitokeza kutokana na uwepo wa uchafu huo," alisema.

Mfinanga aliwataka watendaji ngazi ya kata na mitaa kuendelea kutoa elimu kwa wananchi itakayowawezesha kukabiliana na magonjwa yanayoweza kujitokeza katika kipindi cha msimu wa mvua.

Alisema kuwa elimu hiyo ni pamoja na kuhakikisha wananchi wanajiepusha na utupaji taka ovyo na kuweka maeneo yao safi.

Alisema: "Fanyeni ukaguzi wa mara kwa mara kwenye mikusanyiko ya watu kama vile kwa wafanyabiashara wa sokoni migahawa ya mama na baba lishe, hotelini na maeneo ya kuhifadhia taka lengo ni kupambana na magonjwa ya mlipuko".



# Prof. Kabudi aagiza mbegu za mpunga kutunzwa

**Na Nebart Msokwa,** KYELA

SERIKALI imeagiza wataalamu wa kilimo katika Wilaya ya Kyela mkoani Mbeya, kuhifadhi mbegu za asili za mpunga ambazo zimeipatia sifa wilaya hiyo katika masoko ya ndani na nje ya nchi.

Waziri wa Katiba na Sheria, Prof. Palamagamba Kabudi, alitoa agizo hilo juzi kwenye mkutano wa hadhara na wananchi wa Wilaya ya Kyela ikiwa ni sehemu ya mwendelezo wa ziara ya kikazi ya kutembelea halmashauri zote za mkoa huo.

Alisema mchele kutoka katika wilaya hiyo umekuwa ukitumika katika hoteli za kimataifa kutokana na ubora wake pamoja na harufu nzuri na kwamba umekuwa ukiwaingizia wakulima fedha nyingi.

Alisema katika miaka ya karibuni aina hiyo ya mbegu imeanza kupotea kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo ongezeko la magugu na hivyo kuwalazimu wakulima kuanza kupanda aina zingine za mpunga ambao ubora wake ni mdogo.

"Naomba aina hiyo ya mpunga muitunze ili isipotee kabisa, lakini pia nawaomba wakulima mwendelee kulima aina hii ya mpunga kwa sababu ina soko zuri sana nje ya nchi, ndiyo aina ya mchele ambao unatumika kwenye hoteli za nyota tano duniani," alisema Prof. Kabudi.

Aidha, alisema mbali na aina hiyo ya mpunga pia Wilaya ya Kyela ndiyo inayoongoza duniani kwa kuzalisha kakao bora ambayo imekuwa ikitumika kuzalisha bidhaa mbalimbali ikiwamo chokoleti.

**Aidha, alisema mbali na aina hiyo ya mpunga pia Wilaya ya Kyela ndiyo inayoongoza duniani kwa kuzalisha kakao bora ambayo imekuwa ikitumika kuzalisha bidhaa mbalimbali ikiwamo chokoleti.**

Vilevile, alisema wilaya hiyo inazalisha mazao mengine ya kimkakati ikiwamo michikichi ambayo inatumika kuzalisha mafuta ya mawese pamoja na korosho.

Alisema kutokana na upekee wa wilaya hiyo, serikali imewekeza kwenye uboreshaji wa miundombinu ya usafiri na usafirishaji ili kuwarahisishia wananchi kusafirisha mazao yao.

Alisema serikali imejenga barabara nyingi za lami kwa ajili ya kuunganisha wilaya hiyo na Bandari ya Ziwa Nyasa hasa za Itungi na Ngonga zilizopo wilayani humo na Mbamba Bay iliyopo mkoani Ruvuma kisha kuunganishwa na Bahari ya Hindi kwa njia ya barabara.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera alisema Wilaya ya Kyela ni miongoni mwa wilaya ambazo zimenufaika na miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwemo ya sekta ya kilimo, afya, elimu na miundombinu ya barabara.

Alisema serikali imetoa ruzuku ya miche ya kisasa ya michikichi ambayo inasambazwa kwa wakulima kwa ajili ya kuhamasisha uzalishaji wa zao hilo kwa lengo la kupunguza uagizaji wa mafuta nje ya nchi.

"Lakini kwenye zao la kakao mwaka huu bei imevunja rekodi kwa sababu imepanda kutoka Sh. 2,800 ambayo ilikuwepo awali mpaka Sh. 32,000 bei ambayo imetokana na serikali kuimarisha mfumo wa stakabadhi za ghala," alisema Homera.

Mbunge wa Jimbo la Kyela, Ally Jumbe maarufu kwa jina la 'Kinanasi', aliiomba serikali kukamilisha ujenzi wa Barabara ya Ibanda-Kanjunjumele-Itungi Port kwa kiwango cha lami ili kuwarahisishia wananchi usafiri.

Alisema barabara hiyo ilianza kujengwa na baadhi ya wananchi walibomoa nyumba zao kwa hiyari ili kupisha mradi huo lakini mpaka sasa ujenzi haujendelei na wananchi hawakulipwa fidia.



Waziri wa Katiba na Sheria, Prof. Palamagamba Kabudi (kulia), akizungumza na mmoja wa wakulima wa chikichi wilayani Kyela, mkoani Mbeya alipomtembelea shambani kwake juzi, ikiwa ni mwendelezo wa ziara yake ya kikazi katika halmashauri zote za mkoa wa Mbeya. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Serikali yapewa kongole ujenzi Kituo cha Afya Lupalilo

**Na Elizabeth John,** MAKETE

WANANCHI wa Kata ya Lupalilo wilayani Makete katika Mkoa wa Njombe, wameishukuru serikali kwa kuwajengea kituo cha afya, wakisema kitawasaidia kupunguza adha ya wajawazito kujifungulia njiani.

Walitoa pongezi hizo mwishoni mwa wiki katika mkutano wa hadhara wa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Adolf Mkenda baada ya kuzindua Kituo cha Afya Lupalilo ambapo walisema wamekuwa wakipata shida kwa miaka mingi.

Walisema kabla ya kujengwa kwa kituo hicho walikuwa wanalazimika kutembea umbali mrefu kufuata huduma za afya na hivyo kusababisha baadhi ya wajawazito kujifungulia njiani.

"Tulikuwa tunapata shida kutembea umbali mrefu lakini sasa hivi huduma zinapatikana kwa uhakika, kwa sababu kulikuwa pia na madhara ya wajawazito kujifungulia njiani," alisema Kulwa Mtazamba.

Naye Anthony Mapunda alisema ujenzi wa kituo hicho ni mkombozi kwa sababu huko nyuma walipata adha kubwa kwa kuwa kata hiyo inawatu wengi na kwenda Makete ni mbali hivyo ilikuwa ni ngumu mwananchi wa kawaida kumudu gharama za usafiri.

Katibu Tawala Mkoa wa Njombe, Judica Omary, alisema ujenzi wa kituo hicho utasaidia wananchi kupata huduma za afya kwa karibu na uhakika na hivyo kuondokana na adha ambazo walikuwa wakikutana nazo.

Kwa upande wake, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Adolf Mkenda alisema serikali inaendelea kuboresha miundombinu na huduma za afya sambamba na kuleta vifaa tiba vipya na vya kisasa.

Ofisa Mtendaji wa Kata ya Lupalilo, Sabas Setas alisema kituo hicho cha afya kimejengwa kwa zaidi ya Sh. milioni 500 na kitanufaisha wananchi 4,326.

Alisema kukamilika kwa kituo hicho pia kutasaidia wananchi ikiwamo kupunguza gharama za usafiri kwa wagonjwa wanaokwenda kutafuta huduma za afya katika Hospitali ya Consolatha Ikonda na Hospitali ya Wilaya ya Makete.

# 'Wazazi, walezi msikwepe jukumu la malezi'

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WAZAZI na walezi katika Halmashauri ya Mji wa Makambako mkoani Njombe wametakiwa kuwa karibu na watoto wao na kufuatilia maendeleo yao kitaaluma, badala ya kuwaachia walimu pekee kwa kisingizio cha kuwa na majukumu mengi.

Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii wa Halmashauri hiyo, Lilian Mwelupungwi, alitoa wito huo mwishoni mwa wiki wakati wa Maadhimisho ya Wiki ya Elimu ya Watu Wazima na Jumuishi ambayo yalifanyika katika Shule ya Msingi Idofi iliyoko Kata ya Mlowa.

Alisema makuzi na malezi ya watoto yanategemea zaidi wazazi huku akisisitiza kwa watu wazima ambao hawakupata elimu kuhakikisha wanajua kusoma, kuandika na kuhesabu kupitia mfumo wa elimu ya watu wazima.

"Hizi shughuli zetu zisitufanye tukawakatili watoto, hawa watoto tuwaangalie kwa jicho la ukaribu kwa sabbau wazazi tumekuwa na majukumu ambayo yanatufanya mpaka tunashindwa kuwaangalia watoto kwa ukaribu," alisema Mwelupungwi.

Aidha, aliwataka wazazi kuzingatia malezi ya kidini kwa watoto wao ili kuepukana na matukio ya ukatili hasa ulawiti na ubakaji ambayo yanaathiri jamii, huku akitaka jamii kuacha kuwafungia ndani watoto wenye ulemavu kwa kuwaendeleza kielimu.

Ofisa Elimu Maalumu kutoka Halmashauri ya Mji wa Makambako, Exavelia Mtega, alisema halmashauri hiyo ina wanafunzi wenye mahitaji maalumu 625 ambao wanasoma elimu msingi na 176 wa elimu ya sekondari, huku elimu ya watu wazima ikiwa na wanafunzi 109.

Baadhi ya wananachi ambao walihudhuria katika maadhimisho hayo akiwamo Zaitun Myinga alikiri uwepo wa watu wazima wasiojua kusoma na kuandika katika maeneo yao.



## Serikali: Tutawatunza wazee wasio na ndugu

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imesema inaendeleza jitihada za kuwahudumia na kuwatunza wazee wasio na ndugu wala jamaa katika makao maalum ya wazee yaliyoko Sebleni, Welezo na Limbani.

Hayo yalisemwa na Wazira ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Riziki Pembe Juma, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu Maadhimisho ya Siku ya Wazee Duniani.

Alisema wazee 68 wanatunzwa katika makazi ya wazee wakiwamo 38 wapo Welezo, 12 Sebleni na tisa wapo Limbani Pemba.

Alisema wazee hao wote wanaendelea kupatiwa huduma za kiustawi ikiwamo chakula, mavazi, malazi, matibabu na fedha za kujikimu.

Alisema katika kuendeleza jitihada hizo, serikali imetoa vitambulisho kwa wazee wote Zanzibar wenye umri wa miaka 70 na kuendelea, vyenye lengo la kusaidia upatikanaji wa huduma muhimu za kijamii kwa urahisi, zikiwemo huduma za usafiri wa umma, afya, kuingia kwenye viwanja vya michezo vya serikali na pensheni jamii.

Aidha, alisema kwamba serikali kwa kuona umuhimu na mchango mkubwa wa wazee katika kuleta maendeleo ya nchi iliongeza kiwango cha pensheni jamii kutoka Sh. 20,000 hadi Sh. 50,000 sawa na asilimia 150 kwa wazee wote wenye umri wa miaka 70 na kuendelea.

Alisema hatua hiyo ni miongoni mwa utekelezaji wa Sera ya Hifadhi ya Jamii ya Mwaka 2014 ambayo imeeleza changamoto kubwa inayowakabili wazee ni ukosefu wa usalama wa kipato.

Kadhalika alisema sheria hiyo imeweka miongozo imara inayohakikisha wazee wanapatiwa pensheni kwa kuzingatia vigezo vilivyowekwa.

Hata hivyo, alisema serikali inafanya kila juhudi kupitia Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa kushirikiana na jumuiya na mabaraza ya wazee katika ngazi za mkoa, wilaya na shehia ili kusimamia maendeleo ya wazee nchini.

Alisema hadi Agosti mwaka huu, mabaraza tisa ya wazee yameanzishwa katika ngazi ya wilaya, Unguja na Pemba.

Maadhimisho ya Siku ya Wazee Duniani yatafanyika leo Kisiwani Pemba ambapo Rais wa Zanzibar Dk. Hussein Ali Mwinyi anatarajiwa kuwa mgeni rasmi.

# Wazazi wazipa kipaumbele harusi kuliko maendeleo ya mtoto shuleni

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

OFISA Elimu wa Wilaya ya Kusini Unguja, Mussa Nahodha Makame, amesema anashangazwa kuona baadhi ya wazazi na walezi mkoani humo kuzipa kipaumbele shughuli za harusi kuliko kufuatilia maendeleo ya elimu ya watoto wao shuleni.

Aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati wa Kongamano la Usawa wa Kijinsia lililoandaliwa na mradi wa kuwatengenezea mazingira rafiki ya kujisomea kwa wasichana (KFHI) ambalo limewakutanisha wazazi na walezi.

Alisema baadhi ya wazizi hawana ukaribu na watoto wao hasa wa kike katika kufuatilia maendeleo yao ya kielimu na wamejikita zaidi katika sherehe za harusi.

Makame alisema katika kufikia maendeleo ya mtoto kupata elimu lazima wazazi na walezi wawe mhimili muhimu kwa kuwa karibu na watoto wao.

"Watoto kwa kawaida wanatakiwa kuwa na usimamizi mzuri wa wazazi na walezi na walimu pia kinyume na hapo jamii inaenda kupata viongozi wa ovyo hapo baadaye," alisema. Alisema kuwa wazazi na jamii wanawajibu wa kuwalea watoto wao bila ya kuwabagua kijinsia kwa sababu wote wanahaki sawa katika kupata elimu bila ya ubaguzi wa aina yoyote.

**Kadhalika, aliwataka vijana kuendelea kuwa raia wema, wenye nidhamu na uzalendo pamoja na kufuata malezi na mustakabali mwema.**

Alisema kuwa Wizara ya Elimu na Mafunzo imeweka sheria na miongozo juu ya kuwapatia elimu watoto wote bila ya kuwabagua kwa jinsia zao hivyo wazazi wanawajibu wa kufuata miongozo hiyo.

Kadhalika, alizitaka familia kuwashirikisha watoto wa kike katika kutoa ushauri kwenye ngazi za familia ili kuwa na sauti na kusikilizwa katika kujenga familia bora.

Meneja wa mradi huo kutoka Shirika la KFHI linalofadhiliwa na KOICA, Taewan Park alisema kuwa elimu ya jinsia ni msingi wa kuijenga jamii jumuishi kwa wanawake na wanaume bila ya kujali tofauti zao.

Alisema kuwa kufanya hivyo itakuwa ni fursa nzuri ya kuwaondoshea changamoto hizo kwa kusoma kwa mafanikio na kufikia malengo ya ndoto walizojiwekea.

Ofisa Mtendaji wa Elimu Jumuishi kutoka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Fatma Mbaraka Hashim alisema kuwa wazazi na walezi wanatakiwa kuwa mstari wa mbele katika kuwahimiza watoto wao wa kike kusoma na siyo kuwa na haraka ya kuwaoezesha.



Mjumbe wa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi, Jaji wa Mahakama Kuu, Asina Omar (kushoto), akiangalia namna waandishi wasaidizi na waendesha vifaa vya bayometriki wanavyofanya mazoezi ya uboreshaji kwa vitendo katika kituo cha Walimu Bububu, Wilaya ya Magharibi A Mkoa wa Mjini Magharibi, Zanzibar mwishoni mwa wiki. Zanzibar inaanza uboreshaji wa daftari leo hadi Oktoba 13, 2024 na vituo vitafunguliwa kuanzia saa 2:00 asubuhi na kufungwa saa 12:00 jioni. **PICHA: INEC**

# Serikali yawahakikishia walimu mafunzo ya ujuzi

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Pili wa Rais, Hemed Suleiman Abdulla, amesema Serikali ya Zanzibar kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, itahakikisha walimu wanapata mafunzo wakiwa kazini ili kuwaongezea ujuzi.

Alisema hayo juzi wakati wa ufunguzi wa Kongamano la Maadhimisho ya Siku ya Walimu Duniani yaliyofanyika katika Shule ya Kizimkazi Dimbani Mkoa wa Kusini Unguja.

Alisema ni jambo la muhimu kufanyika kwa maadhimisho hayo yanayolenga kutathmini mafanikio na changamoto za walimu katika kufikia mapendekezo ya hadhi ya walimu yaliyowekwa na UNESCO na Shirika la Kazi (ILO) yanayosisitiza taaluma, mazingira bora, hadhi, heshima na maslahi ya walimu.

Alisema serikali katika kulinda hadhi na maslahi ya walimu imeanzisha Tume ya Utumishi ya Walimu ambayo madhumuni yake ni kusimamia ustawi na kuendeleza kutunza heshima ya walimu pamoja na kusimamia ujenzi wa makazi ya walimu. Aidha, alisema kuwa serikali imekusudia kujenga chuo cha uwalimu ambacho kitatumika kutoa mafunzo kwa walimu na kuwajengea uwezo unaoendana na mabadiliko ya sayansi na teknolojia duniani ili kufundisha kwa ufanisi zaidi.

Hivyo, aliwataka walimu kuitumia vyema fursa ya kukusanyika pamoja kwa kubadilishana uzoefu na maarifa na kuliwekea msisitizo suala la uwajibikaji kazini, maadili mema kwa walimu na wanafunzi na kukumbusha sifa za mwalimu bora.

Hata hivyo alisema serikali itahakikisha inazitatua changamoto zote zinazowakabili walimu ikiwamo malimbikizo ya fedha za likizo na ufiwa.

Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Lela Mohamed Mussa, alisema walimu wana jukumu la kujiongeza kitaaluma na kujiendeleza kielimu ili kuendana na mageuzi ya mfumo wa elimu ambao unatumia zaidi teknolojia na kuwafanya walimu waendane na matakwa ya elimu duniani. Katibu Mkuu wa Chama cha Walimu Zanzibar (ZATU), Haji Juma alisema Siku ya Walimu Duniani inatoa fursa kwa walimu kutafakari mafanikio na changamoto katika sekta ya elimu hasa katika kuinua viwango vya elimu na ustawi bora wa walimu na wanafunzi nchini.

Aidha, aliitaka serikali kuangalia umuhimu wa kuwashirikisha walimu ipasavyo hasa katika ngazi za maamuzi ili kuzidi kuimarisha sekta ya elimu kwa kutoa elimu bora kwa wanafunzi wote wa Zanzibar.

# Ujumuishi wa kifedha kidijitali nchini kuwafikia wakulima

**Na Waandishi Wetu**

KATIKA jitihada za kuboresha sekta ya kilimo nchini, Benki ya CRDB imejipanga kushiriki utekelezaji Mpango wa Uwezeshaji Wakulima Kidijitali nchini kupitia programu ya 'MADE Alliance: Afrika'.

Akizungumza katika Makao Makuu ya benki hiyo jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela, alisema ushiriki wao katika programu hiyo unalenga kuwaunganisha mamilioni ya wakulima wa Kitanzania na huduma za kifedha kidijitali.

Ushiriki wa benki hiyo katika programu ya 'MADE Alliance' upande wa Tanzania ulitangazwa rasmi wakati wa Mkutano Mkuu wa 79 wa Umoja wa Mataifa (UNGA) uliofanyika hivi karibuni jijini New York, Marekani.

Kupitia akaunti yake ya FahariKilimo ambayo ni mahsusi kwa ajili ya wakulima, benki hiyo imekuwa inawaunganisha wakulima na huduma bunifu za kifedha kama vile malipo ya kidijitali, utunzaji akiba, huduma za bima na upatikanaji wa mikopo, jambo ambalo limesaidia kuwapa uwezo wa kuboresha shughuli zao za kilimo.

Kwa sasa, Benki ya CRDB inaongoza kwa ufadhili wa sekta hiyo muhimu, ikiwa imetoa takribani asilimia 60 ya mikopo yote iliyotolewa na taasisi za fedha.

"Ushiriki wetu katika MADE Afrika unaendana na dhamira yetu ya kuwawezesha wakulima kupitia majukwaa ya kidijitali.

"Tumejizatiti kuwapatia wakulima zana wanazohitaji ili kuboresha mbinu zao, kupata mikopo nafuu, na kujenga uwezo wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

"Suluhisho zetu za kidijitali kama SimBanking na mtandao mpana wa CRDB Wakala zinaleta huduma za kifedha karibu na wakulima, zikiwawezesha kuweka akiba, kukopa na kukata bima ya mazao yao kwa urahisi," alisema.

Akielezea kuhusu huduma mahsusi zinazotolewa na benki hiyo kwa ajili ya wakulima, Nsekela alisema huduma zinazotolewa ni pamoja na mikopo ya pembejeo za kilimo, mikopo ya zana za kilimo, mikopo ya ujenzi wa maghala na uwezeshaji kupitia stakabadhi ghalani.

Vilevile, Nsekela alisema benki yao inashirikiana na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) kutoa bima ya afya kwa wakulima na kupitia kampuni tanzu ya CRDB Bank Insurance, inatoa bima ya mazao dhidi ya majanga kama ukame na mafuriko, kuhakikisha wakulima wanajilinda na majanga yanayoweza kujitokeza.

Katika jitihada zake za kukuza ujumuishi wa kifedha, Benki ya CRDB imeendelea kuboresha jitihada zake za kuwafikia wakulima wengi zaidi kupitia programu ya IMBEJU Kilimo inayoendeshwa chini ya taasisi yake ya CRDB Bank Foundation.

"Kubadilisha mfumo wa kifedha wa kilimo kuwa wa kidijitali ni msingi wa kuendeleza kilimo cha kisasa nchini.

"Kupitia mpango wa IMBEJU Kilimo, tunawawezesha wakulima wadogo kwa elimu ya kifedha, suluhisho za kifedha za kidijitali, pamoja na kuwapatia mtaji wezeshi.

"Programu hii inawapa mbinu za kisasa za kilimo huku ikiimarisha ushiriki wao katika huduma za kifedha za kidijitali, kuhakikisha hakuna mkulima anayebaki nyuma," alisema.

CRDB ni benki pekee nchini iliyoweka jukwaa maalum la kujitolea kwa ukamilifu kuwawezesha wakulima kupitia programu za mafunzo.

Kupitia CRDB Bank Foundation, benki hiyo inawapatia wakulima mafunzo muhimu kuhusu ujuzi wa kidijitali, usimamizi wa kifedha na mbinu za kukabiliana na mabadiliko ya hali ya hewa - kuhakikisha wanakuwa na maarifa na zana muhimu kwa mafanikio katika uchumi wa kisasa.

Kama mshirika aliyeidhinishwa wa Mfuko wa Umoja wa Mataifa wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi (UNGCF), benki hiyo pia inawasaidia wakulima kuanza kutumia mbinu na teknolojia zinazozuia madhara ya mabadiliko ya tabianchi.

Kupitia miradi kama TACATDP, benki hiyo inahimiza na kufadhili matumizi ya suluhisho za kisasa kama mifumo ya umwagiliaji, kilimo cha usahihi na mitambo ya nishati ya jua, ambayo inapunguza hatari za tabianchi na kuongeza uzalishaji.

Akizungumza kwa njia ya mtandao, Jon Hauntsaman, Makamu Mwenyekiti na Rais wa Mastercard, alieleza furaha yake juu ya ushirikiano na Benki ya CRDB katika MADE Afrika, akisema:

"Uzoefu mkubwa wa Benki ya CRDB na kujitolea kwao kwa ufadhili wa kilimo kunawafanya kuwa mshirika muhimu katika programu hii.

"Tunafurahia kushirikiana nao katika kuendeleza na kupeleka suluhisho za kidijitali zitakazowawezesha mamilioni ya wakulima kote Tanzania. Utaalamu wao wa kuunganisha huduma za kifedha na teknolojia ya kisasa, pamoja na uhusiano wao wa karibu na jamii za wakulima, unaendana kikamilifu na malengo ya programu hii."

Ushiriki wa Benki ya CRDB katika programu ya MADE Afrika unazidi kuimarisha nafasi yake kama benki kiongozi katika kuboresha sekta ya kilimo nchini Tanzania. Kwa kuwapatia wakulima zana na msaada wanaohitaji ili kufanikiwa, benki ya hiyo inajenga mustakabali mzuri kwa wakulima wa Tanzania na kukuza mchango wa sekta ya kilimo katika uchumi wa taifa.

## KUPOTEA KADI YA PIKIPIKI

Ndugu **ALLY BAKARI NYARI** anatangaza kupotea kwa kadi ya pilipiki yenye namba za usajili **MC 214 DUA.** Na chassis No. **LJECJL03PA004243.** Kwa yeyote atakayeiona anaombwa atoe taarifa kituo cha Polisi kilicho karibu. Amefika Polisi na amepewa Loss Report. Taarifa Polisi: **PHQ/TAN/TAN/9822/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**AMOS MAKABALA MARWA**

Anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye namba za usajili **MC 393 DLE** aina ya **KINGLION.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo jirani yake. Taarifa ya polisi. **PHQ/SHI/KAH/3895/2024.**

## VIWANJA VYA PETROL STATION VINAUZWA DODOMA.

1. kiwanja cha petrol station kipo mtumba, Dodoma mjini ukubwa 3509sqm kina hati na vibali vyote bei **Tsh 320,000,000.**
2. kiwanja cha petrol station kipo manchali, chamwino Dodoma ukubwa **6157 sqm** kina hati bei Tsh 320,000,000
3. Heka 1.5 zinauzwa Tsh 45,000,000,na heka 2.5 zinauzwa Tsh 75,000,000 zipo manchali chamwino Dodoma zinatazama barabara ya dodoma kwenda morogoro hazijapimwa nzuri kwa vituo vya mafuta.

**Mawasiliano: 0655660730**

## KUPOTEA KWA KADI ZA BAJAJI

**GODLOVE SHIWARYAELI MUNISI** anatangaza kupotea kwa kadi za bajaji zenye usajili namba **MC 866 CBM na MC 522 CHU.** Kwa yeyote atakaeziona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR/KIN/214854/2024**

## KUPOTEA KWA VYETI



**AINESS PRUDENCE** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S3272/0002** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **BUHEMBE SECONDARY SCHOOL** mwaka 2012, cheti cha kidato cha sita chenye index namba P0379/0501 kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **MGULANI CENTER (JKT)** mwaka 2019 na cheti cha chuo chenye usajili namba MNMA/BD.EGK/1990/19 kilichotolewa na MWALIMU NYERERE MEMORIAL ACADEMY mwaka 2022. Kwa yeyote atakaeviona atoa taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **phq/dar/tem/215382/2024**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**

**WILAYA MOROGORO**
**LILILOPO MOROGORO**

**MAOMBI MADOGO NAMBA 134 YA 2024**

**YONA LUKAS MAKI....................................MLETA MAOMBI**

**DHIDI YA**

1. **STEPHEN KEBWE**
2. **NYABOSI MARO KYARIGA**
3. **LEONI DYALILI**
4. **GODFREY MWAKALINGA**
5. **PAUL MOSHA....................................WAJIBU MAOMBI**

**WITO/KUITWA SHAURINI KWA**

1. **STEPHEN KEBWE**
2. **NYABOSI MARO KYARIGA**
3. **LEONI DYALILI**
4. **GODFREY MWAKALINGA**

Popote mlipo mnaarifiwa mfike katika Baraza la Ardhi na Nyumba Wilaya Morogoro tarehe 22/10/2024 mbele ya Mwenyekiti M. KHASIM nyie wenyewe au mtume muwakilishi wenu bila kukosa ambapo maombi yamepangwa kutajwa. Endapo hamtahudhuria maombi yatatajwa na kusikilizwa upande mmoja dhidi yenu na kutolewa uamuzi.
Imetolewa kwa MKONO wangu na MUHURI wa Baraza leo tarehe 1 mwezi Oktoba, 2024.

**M. KHASIM**
**MWENYEKITI.**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya**
**DODOMA MJINI**

**Kituo cha MJINI** **Mkoa DODOMA**

**Usimamizi wa mirathi Na 76/2024**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU AISHA GHOTHI WA BARABARA 9 KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA SAID AHMED GHOTH**

**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 09 Mwezi 10 Mwaka 2024 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
*Wosia wa marehemu huyo upo Mahakamani na waweza kukaguliwa.
*Marehemu hakuacha wosia
*Futa isiyohusika
Imetolewa leo Tarehe 02 Mwezi 10 Mwaka 2024

---

**NACHAGO GENERAL ENTERPRISES LIMITED**
**Incorporation Number 123999**
**(The "Company")**

**NOTICE OF THE FINAL MEETING OF MEMBER'S VOLUNTARY WINDING UP OF THE COMPANY TO TAKE PLACE AT 08:00 HOURS EASTERN AFRICA TIME (EAT) ON 5th DAY OF NOVEMBER 2024**

**Notice of the final meeting under section 345(1) and (2) of the companies Act 212 R.E 2022**

**TO THE MEMBERS AND GENERAL PUBLIC**

Notice is hereby given that the liquidator intends to convene the final general meeting in respect of **NACHAGO GENERAL ENTERPRISES LIMITED** which will be held at Johnsons Villas Hotel, Kilimanjaro on 5th November 2024 08:00hours.

The purpose of the meeting is for Liquidator to lay accounts of winding up showing the manner in which the winding up of the company has been conducted and its properties disposed of giving other explanations hereto

Signed at Dar es salaam this 3rd October 2024

**Sila Siya Kisanga**
**The Liquidator**

---

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**MASJALA NDOGO YA TEMEKE**
**(TEMEKE KITUO JUMUISHI HUDUMA ZA MAHAKAMA MIRATHI NA NDOA)**

**MIRATHI NA 24126 YA MWAKA 2024**

**MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU**

**JAYANTILAL NAGINDAS MEISURIA**
**MAYUR KANTILAL MEISURIA .....................MWOMBAJI**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(Kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia shauri hili katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua ya usimamizi wa mirathi kwa mwombaji hapo juu.

Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 29 mwezi 10, 2024. Saa 08:00 Asubuhi. Siku ambayo shauri hili limepangwa kusikilizwa mbele ya Mhe. A.A Omari

Imesainiwa Dar Es Salaam, Leo tarehe 03 mwezi 10, 2024

NAIBU MSAJILI

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 67410 OF 2024**

**In the matter of the late JEROME JOSEPH KIWIA**

**And**

**In the Matter on an Application for letters of administration by HILDEGARDA JEROME KIWIA**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of probate Rules GN NO. 369 of 1963)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased person are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letter of Administration is made to the above named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 08 Day of 11..........................2024


..........................................................................
**Petitioner**
**Presented for filling this 04 Day of 10..........................2024**

RESIDENT MAGISTRATE

## HABARI KIMATAIFA

# Naibu Rais Kenya aomba radhi

**Na Maulid Mmbaga**


Naibu Rais wa Kenya, Rigathi Gachagua. **PICHA: MTANDAO**

NAIBU Rais wa Kenya, Rigathi Gachagua, ameomba msamahama ikiwa ni siku moja kabla ya kujitetea mbele ya bunge kwa saa mbili kuhusu tuhuma za utovu wa nidhamu, ukiukaji wa katiba, na kujilimbikizia mali kinyume cha sheria tangu aingie madarakani.

Gachagua aliomba radhi jana wakati wa ibada ya kitaifa ya maombi yaliyofanyika jijini Nairobi, na kusema kama kuna aliyemkosea akiwa Naibu Rais, amsamehe kutoka moyoni.

Pia alimwomba msamaha Rais William Ruto, wabunge waliowasilisha hoja katika Bunge la Taifa ya kumwondoa madarakani, na Wakenya kwa makosa aliyoyafanya.

"Ningependa kumwambia kaka yangu Rais William Ruto, kama katika juhudi zetu za kufanya kazi, nimemkosea, tafadhali anisaidie kwa moyo wake kunisamehe. Ikiwa mke wangu na mtoto wangu katika majukumu yao wamemkosea basi awasamehe pia," alisema Gachagua.

Kiongozi huyo aliongeza kuwa anachokifanya ni kuthamini waliompigia kura yeye na Rais Ruto katika mchakato wa kuingia madarakani.

"Unakuta katika kuthamini watu wetu na uungwaji mkono waliotupatia rais na mimi, pengine matamshi yetu yalikukosesha raha, hatukuwa na maana mbaya, tulikuwa tunathamini watu waliotupigia kura, ukihisi tulikusugua, njia mbaya, tafadhali tafuta moyoni mwako ili unisamehe," alisema Gachagua.

Aidha Gachagua alikanusha makosa yoyote kumuhusu akisema ni uwindaji wa wachawi wa kisiasa kwa sababu ya kuunga mkono uwanja wake wa Mlima Kenya.

Hata hivyo, ushiriki wa umma katika kuondolewa mashtaka umekuwa ukiendelea, lakini Wakenya wengi wanataka Gachagua na Ruto kuondoka wote ofisini.

### MTAZAMO WA JAMII

Kwa upande wa maoni ya wananchi baadhi yao wametaka kufutwa kazi kwa Rais Ruto na naibu wake Gachagua, wakieleza kuwa hakuna njia ambayo mtu anaweza kushtakiwa na mwingine kuachwa.

Katika ushirikishwaji wa umma kuhusu kuondolewa kwa Gachagua Wakenya walionyesha kutoridhishwa kwao na serikali ya Kenya Kwanza "Ikiwa tout itakufa, dereva afe pia. Waende wote nyumbani," mkenya mmoja alisikika akisema.

Mtu mmoja alisema kitendo cha kumshtaki mmoja wao hakutakuwa na maana, kwani walichaguliwa katika ofisi pamoja.

**Ilielezwa kuwa jumla ya wabunge 291 kati ya 249 wa Bunge la Taifa walisaini hoja ya kumshtaki na kumng'oa madarakani Naibu huyo.**

"Waambie hatuwezi kutenganisha harusi yao. Ikiwa tutawatenganisha basi wote waende nyumbani," Mkenya mwingine alisema.

Hayo yanajiri baada ya baadhi ya wabunge wa eneo la Mlima Kenya kujiondoa katika kuunga mkono hoja ya kumtimua Naibu Rais wa taifa hilo Gachagua.

Ilielezwa kuwa wabunge ambao awali waliunga mkono hoja ya Gachagua kuondolewa madarakani lakini baadaye wakabadili msimamo wao ni Mbunge wa Tetu, Geoffrey Wandetu, Mbunge wa Nyeri, Rahab Mukami na Mbunge wa Kieni, Njoroge Wainaina.

Mbunge wa Nyeri, Rahab Mukami alisema alitambua kuwa mashtaka dhidi ya Gachagua ni masuala ambayo yeye na bosi wake wanaweza kutatua kupitia majadiliano.

Akirejelea matamshi ya Mukami, Wandetu alisema alishauriana na wapigakura wake, ambao walimweleza kuwa kumshtaki Gachagua sio kipaumbele.

Wabunge hao pia walimtaka Gachagua kuomba msamaha kutoka kwa Rais William Ruto ili kutatua tofauti zozote baina yao.


Rais William Ruto,

Mbunge wa Embu, Pamela Njoki pia alibadilisha msimamo wake akisema ingawa awali aliunga mkono hoja hiyo, alitafakari upya baada ya kushauriana na wakazi wa Embu.

### MAWAKILI 20 KUMTETEA

Awali ilielezwa kuwa naibu rais huyo ameandaa timu ya mawakili 20 wa ngazi za juu kwa ajili ya kutetea kesi yake mbele ya wabunge. Na kwamba anayeongoza kundi hilo ni Wakili Mkongwe Mwandamizi Paul Muite pamoja na Tom Macharia, Amos Kisilu, Elisha Ongoya na Victor Ogeto.

Ilielezwa kuwa timu ya wanasheria inanuia kuegemeza utetezi kwa Gachagua kuhusu jinsi ushirikishwaji wa umma ulivyotekelezwa na upendeleo unaodaiwa kuwa wa Spika Moses Wetang'ula na naibu wake Gladys Shollei kuelekea kuondolewa mashtaka.

Wakili Ogeto alidokeza kuwa Wakenya walivamiwa ili kuwasilisha maoni yao, akidai kuwa nchi haikuwa tayari kushtakiwa. "Unatoa notisi usiku, watu wanaamka sasa, kuhusu nini kifanyike mwisho wa leo. Je, ni haki gani," alisema Ogeto.

Zaidi ya hayo, wakili huyo alifichua kuwa wangeomba kujiuzulu kwa Wetang'ula na Shollei baada ya kueleza hadharani misimamo yao ambayo ilitafsiriwa kuwa inaunga mkono kuondolewa kwa Gachagua.

Ogeto aliongeza kuwa, kwa kuzingatia upendeleo wa Spika na naibu wake, haitakuwa busara kwao kusimamia mchakato ambao mshtakiwa anataka kusikilizwa kwa haki.

"Kwa ajili ya haki, maofisa wakuu wawili wajitoe kwani mjadala huu unakuja," alisema.

### MCHAKATO USITISHWE

Wakati hayo yakijiri, ilielezwa kuwa Gachagua amepeleka ombi mahakamani, ambalo aliwasilisha kusitisha mchakato wa kumwondoa madarakani, akikosoa mchakato huo, akisema baadhi ya kanuni muhimu zilipuuzwa.

Pia alisema kuondolewa kwake kutabatilisha wosia wa Wakenya walio wengi waliompigia kura kama naibu wa rais.

Bunge la Taifa hilo lilianza mchakato wa kumshtaki na kumng'oa madarakani Naibu Rais, baada ya Spika Moses Wateng'ula kuzikubali hoja 11 zilizowasilishwa na Mbunge wa Kibwezi West, Mwengi Mutuse.

Ilielezwa kuwa jumla ya wabunge 291 kati ya 249 wa Bunge la Taifa walisaini hoja ya kumshtaki na kumng'oa madarakani Naibu huyo.

Ibara ya 150 ya Katiba ya Kenya inaeleza masharti ya kuondolewa kwa Naibu Rais, ikiwa ni pamoja na ukiukwaji wa sheria na kutokuwa na uwezo wa kutekeleza majukumu yake.

Licha ya hoja ya kumshtaki lazima iungwe mkono na angalau theluthi moja ya wabunge 117 katika Bunge ili taratibu zianze ikiwa Bunge la Kitaifa na Seneti wataridhia kwa theluthi mbili kiwango ambacho kilishakamilika na kupitiliza. **Chanzo Citizen, KTN**

## HABARI MICHEZO

# RAIS SAMIA AWAJAZA MAMILIONI 'KNOCKOUT YA MAMA' MAGOMENI

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan, ametia mkono katika maendeleo ya mchezo wa masumbwi nchini kwa kuamua kutoa zawadi kwa Watanzania wote walioshinda katika mapambano ya ngumi yanayofahamika kama 'Knockout ya Mama', ambayo yalifanyika katika Ukumbi wa City Centre Hall Magomeni, Usalama, jijini Dar es Salaam.

Katika mapambano hayo, mabondia wa Tanzania wasiopungua nane walipanda ulingoni kucheza na wapinzani wao kutoka nchi mbalimbali zikiwamo Ufilipino, Ghana, Afrika Kusini, Uganda na Angola.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam, Mratibu wa Uzalishaji na Matangazo wa Mafia Boxing Promotion, Omary Clayton, alisema Rais Samia ameingiza mguu kwenye mchezo wa masumbwi wakati huu ambao wadau na mabondia wanakiu ya kufanya makubwa na kuitangaza nchi katika nyanja za kimataifa.

**Alisema Rais Samia aliamua kutoa zawadi nono kwa mabondia Watanzania watakaopata mikanda pamoja na wale watakaoibuka washindi katika mapambano ya kawaida.**

"Mama amekuja kwenye masumbwi kwa nguvu zote, ambapo kila Mtanzania aliyeshinda katika pambano lake ameshikwa mkono tukiamini huu ni mwendo mzuri katika juhudi za kuuinua mchezo wa ngumi nchini kwetu.

"Kwa ujumla yamefanyika mapambano 11, ambayo nane ni ya kimataifa, huku matatu yaliyosalia ndio yameshirikisha Watanzania watupu ambapo pia zawadi ya Knockout ya Mama ilihusika," alisema Omary.

Baadhi ya mabondia wa Tanzania waliopata zawadi ya Rais Samia ni pamoja na Issa Nampepeche aliyemchapa kwa Knockout mpinzani wake, Joseph Masunga na kujinyakulia Sh. milioni tatu, Mchanja Yohana alipata Sh. milioni 1.5 kwa kumpiga kwa pointi mpinzani wake, Michael Aban wa Ghana.

Wengine ni Mtanzania Salmin Kassim aliyeibuka na Sh. milioni tatu kwa kumpiga kwa Knockout mpinzani wake, Non James wa Ufilipino, huku Mtanzania mwingine Ibrahim Mafia yeye akizoa Sh. milioni saba baada ya kushinda mkanda wa WBC Africa dhidi ya bondia kutoka Ghana, Enoch Tetty katika pambano la raundi tisa.

Naye Mtanzania Kalolo Amiri alizawadiwa Sh. milioni 1.5 za Rais Samia kwa kushinda kwa pointi dhidi ya mpinzani wake, Bono Koane wa Afrika Kusini, huku Mtanzania mwingine, Said Mohamed, maarufu kama Chino akiibuka na mkanda wa IBA Intercontinental Championship kwa kumchapa kwa pointi mpinzani wake Kusanda Komanisa wa Afrika Kusini na kuondoka na Sh. milioni tano za Knockout ya Mama.



Bondia Said Mohamed 'Chino' akiwa mwenye furaha baada ya kushinda Mkanda wa IBA International Championship kwa kumchapa mpinzani wake, Lusanda Komanisa, raia wa Afrika Kusini kwa pointi, katika pambano lililofanyika jijini Dar es Salaam Jumamosi iliyopita. Kwa ushindi huo amezawadiwa Sh. milioni tano kutoka kwa Rais Samia Suluhu Hassan. **MPIGAPICHA WETU**

# *Simba Queens na usajili mkubwa dirisha dogo*

**Na Adam Fungamwango**

KlABU ya Simba, inatarajia kufanya usajili mkubwa kwenye kikosi cha timu ya soka ya wanawake katika kipindi cha dirisha dogo la usajili kwa ajili ya kukiboresha baada ya kuonekana kuanza kushuka kiwango.

Habari kutoka ndani ya klabu hiyo, zinasema kuwa pamoja na mambo mengine, wameona kikosi hicho kimeanza kupungua nguvu kiasi cha kushindwa kufanya vema kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika Kanda ya CECAFA na kuamua kuachana na aliyekuwa kocha wa timu hiyo, Juma Mgunda.

Kipigo cha mabao 4-3 kwa mikwaju ya penalti Jumatano iliyopita dhidi ya Yanga Princess, Uwanja wa KMC Complex, Mwenge, Dar es Salaam, katika nusu fainali ya Ngao ya Jamii, kimewashtua na kuona ipo haja ya kufanya usajili kwani hivi sasa kuna wachezaji wachache sana ambao wanaweza kuwapo kwenye kikosi cha kwanza, lakini wengi viwango vyao vimeshuka.

Taarifa zinasema Simba Queens inatarajia kusajili golikipa mwingine mwenye uwezo zaidi, baada ya kuonekana waliopo kushuka viwango kama Rufa Carolyne aliyefanya makosa mengi nchini Ethiopia kwenye mechi za CECAFA kusaka kucheza fainali za Ligi ya Mabingwa Afrika, na Janeth Shija, ambaye alidaka katika mechi ya dabi.

"Tuna kazi ya kufanya, ni wachezaji wachache tu waliosajiliwa ndiyo wapo kwenye ubora, wengi uwezo umeshuka, hapa kuna Vivian Corazone, Precious Christoper, Elizabeth Wambui, Jentrix Shikangwa, Asha Djaffar na wengine wachache, " alisema mtoa taarifa.

Meneja Habari na Mawasiliano wa Klabu hiyo, Ahmed Ally, amesema umekuwa ni mwanzo mbaya ambao unawalazimisha kutuliza akili na kuangalia kwa nini wamefeli mara mbili, ili wakianza ligi wawe wamesawazisha makosa yao.

"Tulifeli kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika Ukanda wa CECAFA, tumeshindwa kufikia malengo na sasa kwenye Ngao ya Jamii, tunajua tumekosea wapi, pamoja na mambo ya vibali vya wachezaji, lakini kuna eneo tutarekebisha ili tuanze ligi kwa kishindo," alisema.

# Kocha KVZ FC aachia ngazi

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

ALIYEKUWA Kocha Mkuu wa KVZ FC, Ali Mohmmed Ameir, amebwaga manyanga ya kuendelea kuinoa timu hiyo baada ya kudumu kwa msimu mmoja.

Timu ya KVZ FC imekuwa na mwendelezo mbovu wa matokeo ya sare katika michezo mitano iliyocheza ikishinda mmoja na kutoka sare nne. Awali, akizungumza na gazeti hili kocha huyo alisema ameamua kuchukua uamuzi huo kutokana na kubanwa na majukumu yake ya kikazi na familia.

"Nimeandika barua kwa uongozi wa KVZ FC kuomba kupumzika, kutokana na majukumu ya kikazi niliyokuwa nayo sitokuwa na muda mzuri wa kuishughulikia timu," alisema.

Kwa mujibu wa taarifa kutoka kwa ofisa habari wa timu hiyo, Abduljalili Mohmed, amekiri uongozi wa KVZ FC kupokea barua hiyo na kuridhia ombi la kocha wao huyo.

# Peter ampania TKO Homa ya SGR

**Na Shufaa Lyimo**

BONDIA Chipukizi, Adam Peter, wa Dar es Salaam, ametamba ataibuka na ushindi wa TKO akiwa ugenini dhidi ya mpinzani wake, Karim Omary kutoka Mikese, kuelekea katika pambano la Homa ya SGR litakalofanyika Oktoba 25, mwaka huu, kwenye Ukumbi wa Tanzanite mkoani Morogoro.

Akizungumza na Nipashe jana, alisema atakwenda mkoani humo kuendeleza rekodi yake ya ushindi kwa kumtwanga mpinzani wake huyo.

"Ninaendelea kujifua kuhakikisha ninakwenda kuendeleza rekodi yangu kwa kumpiga Karim ambaye ninaamini siku hiyo hawezi kufurukuta kwangu," alisema Peter.

Bondia huyo aliweka wazi kuwa kutokana na mazoezi anayoendelea kuyafanya akiwa chini ya Kocha wake Mkuu, Ally Machuani, yatamsaidia kupata ushindi siku hiyo.

Kwa upande wake, Machuani, alisema hana wasi wasi na bondia wake kwani anafahamu uwezo wake.

"Kijana wangu hana utani na mtu akiwa ulingoni kwa kuwa anafahamu wajibu wake ni kuwapa burudani mashabiki kwa kumpiga mpinzani wake, alisema Machuani.

Lengo la pambano hilo ni kuunga mkono juhudi zinazofanywa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan, kwa kutambua mchango wa maendeleo ya nchi kupitia mchezo wa ngumi.

## ZISIKUPITE

### RONALDO AMTAKA DE BRUYNE

MSHAMBULIAJI wa Al-Nassr na Ureno, Cristiano Ronaldo, 39, anahimiza klabu hiyo ya Saudi Arabia kumsajili kiungo wa kati wa Ubelgiji, Kevin de Bruyne, 33, wakati mkataba wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33, utakapomalizika na Manchester City msimu ujao. ***(Mundo Deportivo)***

### ALONSO ATAKIWA UNITED

KLABU ya Manchester United ina nia ya kumteua kocha wa Bayer Leverkusen, Xabi Alonso, kuchukua nafasi ya Erik ten Hag na wako tayari kumsubiri kiungo huyo wa zamani wa Liverpool hadi msimu wa majira ya joto. (***Todofichajes***)

### TORRES AWINDWA TRAFFORD

MLINZI wa Aston Villa, Pau Torres, analengwa na Manchester United, ambao wako tayari kutoa karibu pauni milioni 42 kwa mlinzi huyo wa Hispania mwenye umri wa miaka 27. ***(Fichajes)***

### SALAH ATAKIWA SAUDIA

KLABU ya Klabu ya Saudi Pro League, Al-Ahli inataka kumsajili mshambuliaji wa Misri, Mohamed Salah, 32, na mwenzake wa Liverpool, Virgil van Dijk mwenye miaka 33, wakati mikataba yao itakapomalizika mwishoni mwa msimu huu. ***(Caught Offside)***

### LEWANDOWSKI KUONGEZA

MSHAMBULIAJI wa Poland, Robert Lewandowski, 36, ana chaguo la kuongeza mkataba wake na Barcelona hadi msimu ujao wa majira ya joto ikiwa atafikia vigezo fulani. ***(Sport)***

### FATI KWA MKOPO TENA

BARCELONA inafikiria kumtoa kwa mkopo Januari mshambuliaji wa Hispania, Ansu Fati, 21, ambaye alikuwa na Brighton msimu uliopita. ***(Sport)***

### NKETIAH AFUNGUKA

MSHAMBULIAJI wa England, Eddie Nketiah, 25, amesema aliondoka Arsenal na kujiunga na Crystal Palace msimu wa majira ya joto ili kupata "fursa ya kuwa uwanjani na kuimarika". ***(Independent)***

### DIAZ KUONGEZA MKATABA

LIVERPOOL inatarajiwa kufanya mazungumzo na winga wa Colombia, Luis Diaz, 27, kuhusu mpango wa kuongeza mkataba wake hadi 2027 kutokana na mwanzo wake mzuri msimu huu. ***(Football Insider)***

### LARSSON AFUATILIWA

KLABU kadhaa zinamfuatilia winga wa Eintracht Frankfurt kutoka Sweden, Hugo Larsson, 20. ***(Fabrizio Romano)***

### DIBLING ASHAWISHIWA

KLABU ya Southampton inatumaini kumshawishi kiungo wa kati wa England, Tyler Dibling mwenye umri wa miaka 18, kusaini mkataba mpya huku Manchester United wakionesha nia ya kutaka kumnunua. ***(GiveMeSport)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# POGBA AFUNGUKA KUSHINDA RUFANI

## Sasa huru kurejea uwanjani Juventus Machi mwakani, hii ni baada ya CAS...

**PARIS,** Ufaransa

KIUNGO wa Klabu ya Juventus, Paul Pogba, ambaye alifungiwa kujihusisha na soka kwa kipindi cha miaka minne, amepunguziwa adhabu hiyo mpaka miezi 18 baada ya kufanikiwa kukata rufani katika Mahakama ya Usuluhishi wa Michezo, CAS.

**Nyota huyo raia wa Ufaransa alikumbwa na adhabu hiyo Agosti mwaka jana baada ya kupimwa na kukutwa na kiwango cha juu cha homoni ya Dehydroepiandrosterone ambazo huongeza nguvu mwilini na zimepigwa marufuku michezoni.**

Akizungumza baada ya kupunguziwa adhabu hiyo, Pogba alisema; "hatimaye jinamizi limeondoka na naweza kutazama mbele kutimiza malengo yangu tena na tena, sikuwahi kukiuka kanuni za kupambana kuzuia dawa za kusisimua misuli, nacheza kwa uaminifu na ninaishukuru mahakama kwa kusikiliza maelezo yangu."

"Hii imekuwa ikinisumbua sana kwenye maisha yangu kila kitu nilichofanya kazi kwa bidii kukipata kimesimamishwa. Nawashukuru wote kwa upendo na ushirikiano wenu kwa mara nyingine."

"Nasubiri kwa hamu kurejea tena uwanjani" alisema Pogba kwenye mahojiano aliyoyafanya muda mchache baada ya kushinda rufani yake na kupunguziwa adhabu.

Pogba ambaye alianza kuitumikia adhabu hiyo tangu Septemba 2023, atakuwa huru kurejea uwanjani Machi 2025 na anatarajiwa kuanza mazoezi na klabu yake ya Juventus Januari kwa ajili ya kurejea uwanjani kwa mara nyingine.



# CARVAJAL AIPA PIGO MADRID

**MADRID,** Hispania

BEKI wa Real Madrid, Dani Carvajal, amethibitika kuumia goti katika ushindi wa mabao 2-0 wa timu yake kwenye Ligi Kuu Hispania, LaLiga, dhidi ya Villarreal Jumamosi.

Mchezaji huyo wa Kimataifa wa Hispania, alitolewa nje katika muda wa nyongeza mwishoni mwa kipindi cha pili baada ya kuumia goti alipoenda kuucheza mpira wa juu na kugongana na winga wa Villarreal, Yeremy Pino.

Carvajal baadaye alichapisha kwenye Instagram akithibitisha jeraha hilo la goti, na kuongeza kwamba atahitaji kufanyiwa upasuaji na kuwa nje ya uwanja kwa miezi kadhaa. Akizungumza baada ya kumalizika kwa mchezo huo, kocha Carlo Ancelotti alisema wachezaji wa Real Madrid walikuwa na "huzuni na wasiwasi" kwa mwenzao.

"Inaonekana kama jeraha kubwa la goti, linapaswa kutathminiwa katika saa chache zijazo," alisema Ancelotti katika mkutano wake na waandishi wa habari baada ya mechi.

"Nyumba ya kubadilishia nguo ina huzuni, na ina wasiwasi. Kitu kilitokea ambacho tunatamani kisingetokea. Inatokea, kwa ratiba hii. Kwa bahati mbaya imetokea kwa mchezaji muhimu sana kwetu."

Carvajal aliorodheshwa kwenye tuzo ya Ballon d'Or ya 2024 baada ya msimu wa 2023-24 ambao ulimshuhudia akishinda LaLiga na Ligi ya Mabingwa Ulaya akiwa na Real Madrid, na kisha kubeba taji la Euro 2024 akiwa na Hispania.

"Yeye ni mchezaji muhimu kwetu na uzoefu wake, umakini wake, na taaluma yake," alisema Ancelotti.

"Ni wazi ana huzuni na amekatishwa tamaa, lakini hakuna mengi ya kufanya. Tutaona kile ambacho tathmini ya matibabu inasema, na kisha tufikirie juu ya kupona kwake."

Federico Valverde alikuwa ameiweka Madrid mbele katika kipindi cha kwanza huko Santiago Bernabeu Jumamosi, na Vinicius Junior akaongeza bao la pili la kuvutia baada ya kipindi cha mapumziko, lakini ushindi wa Madrid ulifunikwa na jeraha la Carvajal katika muda wa nyongeza.

"Inaumiza," Valverde alisema. "Mwishowe, matokeo si jambo muhimu zaidi, afya ya Carva ndiyo muhimu."

Ancelotti pia aliulizwa kuhusu utimamu wa Vincius, baada ya kutolewa nje dakika ya 79 kutokana na tatizo la bega.

"Yeye ni mgumu," alisema Ancelotti.

Muitaliano huyo alisema ni mapema mno kufikiria iwapo Madrid wanaweza kulazimishwa kusajili beki wa kulia, huku Lucas Vazquez akiwa ndiye mbadala pekee wa Carvajal kwenye kikosi cha kwanza.

"Hii si siku," alisema. "Tuna imani kubwa na Lucas Vazquez. Wakati huu wa mapumziko tutakuwa na muda wa kulizungumzia. Soko limefungwa, hakuna chaguzi nyingi."

Ushindi wa Madrid uliwaweka sawa kwa pointi 21 na viongozi Barcelona, ambao jana Jumapili walikuwa wanacheza na Alaves.

# Kovacic aelezea maisha City bila Rodri

**MANCHESTER,** England

MATEO Kovacic amesema Manchester City wanahitaji kuzoea maisha bila Rodri baada ya kufunga mabao mawili katika ushindi wao wa mabao 3-2 dhidi ya Fulham kwenye Ligi Kuu England Jumamosi.

Man City walilazimishwa kufanyia kazi pointi tatu kwenye Uwanja wa Etihad, huku Andreas Pereira akiwaweka Fulham mbele katika kipindi cha kwanza kabla ya mabao mawili ya Kovacic kuwasaidia wenyeji kupata bao la kuongoza dakika ya 45.

Bado kulikuwa na wakati kwa Jeremy Doku na Rodrigo Muniz kufunga mabao, lakini ushindi huo unamaanisha City inasalia pointi moja tu nyuma ya vinara wa ligi Liverpool.

Pia wako sawa na Arsenal, wanaokaa mbele katika nafasi ya pili wakiwa wamefunga mabao zaidi.

Mchezaji huyo wa Hispania, Rodri hayumo katika kampeni za 2024/25 baada ya kupata jeraha baya la goti mwezi uliopita na kuwa pigo kubwa kwa matumaini ya City kushinda taji la ligi kwa mara ya tano mfululizo.

Akizungumza baada ya ushindi wa Jumamosi, Kovacic alifichua: "Ninacheza pale katikati kwa sasa na bila shaka tunahitaji kuziba pengo la Rodri. Nafikiri timu yoyote ingemkosa mchezaji ambaye yuko, na tunamtakia ahueni ya haraka na tunatumaini atarejea akiwa katika hali nzuri iwezekanavyo.

"Kwa sasa tunapaswa kuzoea na kwa hakika kocha ana chaguzi nyingi ili tuweze kuzunguka.

"Ulikuwa mchezo mgumu kama kila mchezo wa Ligi Kuu, huwa tunasema hakuna michezo rahisi, tulitawala mwanzo tukashindwa kufunga, tukaruhusu goli kisha tukarudi haraka, mwisho tukashinda na ulikuwa mchezo mgumu dhidi ya mpinzani akiwa katika hali nzuri."

Akimzungumzia Kovacic, kocha Pep Guardiola alisema: "Yeye si mfungaji bora, lakini labda aliona ni mabao mangapi Rodri amefunga katika nafasi hiyo na alifanya. Alifunga mabao mawili ya ajabu."

Mechi ya kwanza ya City baada ya mapumziko ya kimataifa ya Oktoba ni safari dhidi ya Wolves, ambao wapo mkiani mwa jedwali baada ya mechi saba.

# Slot: Alisson kuwa nje kwa wiki chache

**LIVERPOOL,** England

ARNE Slot anahofia jeraha la msuli wa paja alilopata Alisson katika ushindi wa bao 1-0 wa Liverpool dhidi ya Crystal Palace litamfanya kuwa nje kwa "wiki chache."

Liverpool walipata pointi baada ya Diogo Jota kufunga dakika ya tisa, lakini watakabiliwa na wasiwasi juu ya Alisson na kiungo Alexis Mac Allister, ambaye nafasi yake ilichukuliwa wakati wa mapumziko baada ya kuhisi tatizo kwenye paja lake.

Alisson alikosa kwenye ushindi wao wa mabao 3-0 dhidi ya AFC Bournemouth kutokana na jeraha, na alilazimika kutoka nje katika dakika ya 79 ya safari yao ya Selhurst Park baada ya kuumia msuli wa paja.

Kipa chaguo la tatu Vitvzslav Jaros alichukua nafasi ya Alisson na kuichezea Liverpool kwa mara ya kwanza baada ya kipa chaguo la pili Caoimhin Kelleher kukosekana kutokana na ugonjwa katika mechi yao na Palace.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32, baadaye alionдolewa katika mechi zijazo za Brazil za kufuzu Kombe la Dunia, ugenini Chile Alhamisi wiki hii, na nyumbani kwa Peru siku tano baadaye.

Liverpool inakabiliwa na msururu wa mechi baada ya mapumziko ya kimataifa, na Slot anahofia Alisson atakosa kucheza huku wakiwakaribisha Chelsea Oktoba 20 na kisha kusafiri hadi RB Leipzig Oktoba 23, mwaka huu kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

"Ikiwa mchezaji ataondoka kama anavyofanya, hiyo inamaanisha kuwa hayupo kwenye kikosi cha Brazil, na sitarajii kuwa katika mchezo wa kwanza baadaye," alisema Slot. "Itachukua wiki chache nadhani."

Huku Alisson akiwa hayupo, Slot atamgeukia Kelleher kuziba nafasi yake, licha ya kuja kwa Jaros mwishoni mwa ushindi wao wa sita katika mechi saba za Ligi Kuu England msimu huu.

"Alisson ndiye namba moja wetu, mlinda mlango bora zaidi duniani kwa hiyo ni pigo anapojeruhiwa yeye na timu," alisema Slot.

"Tuna chaguo la pili ambalo tayari ni zuri. Caoimhin tayari ameshaonesha hilo, ndiyo maana Caoimhin ni namba mbili na mara ya mwisho, Alisson aliumia, nilicheza na Caoimhin.

Kiungo wa kati wa Argentina Mac Allister alitolewa wakati wa mapumziko.

HABARI MICHEZO

## Simba na bajeti ya bil. 28/-

INATOKA UK. 24

fitna inaondoa baraka ndani ya klabu yetu, na niwaambie watu, Simba si mnyama mkubwa zaidi, si mnyama mwenye mbio zaidi, lakini anabaki kuwa mfalme kutokana na ujasiri wake, tuoneshe ukubwa wetu ki vitendo, mimi nipo nanyi," alisema Dewji huku akishangiliwa na wanachama wa klabu hiyo.

**Jaji Mihayo ateuliwa Mjumbe Bodi ya Wadhamini**

Katika hatua nyingine, Mwenyekiti wa klabu hiyo, Murtaza Mangungu, mbele ya wanachama alipendekeza jina la Jaji Mstaafu, Thomas Mihayo, kuwa mjumbe wa bodi ya wadhamini ambapo wanachama wa klabu hiyo kwa kauli moja walimpitisha.

## Bacca apania kuitungua Simba




INATOKA UK. 24

tena bao, Alhamisi iliyopita, Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam, Yanga iliposhinda mabao 4-0, dhidi ya Pamba Jiji FC.

"Wale waliokuwa wanadhani mimi natania nadhani wameanza kuamini, kama nilivyoweka ahadi yangu, nadhani huu ni mwanzo tu, unajua baada ya kufunga bao moja kule Mbeya, akili yangu sasa nataka kufunga bao kila mchezo unaokuja, na utakaofuata unajua tunacheza na nani Oktoba 19, nataka pia kufunga bao," alisema beki huyo ambaye pia anaichezea timu ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars.

Mchezaji huyo ambaye kwa sasa yupo kambini na Stars, alisema angekuwa na mabao matatu kama si kukatazwa kwenda kupiga penalti katika mchezo dhidi ya Pamba Jiji.

"Unaona hata ile penalti ilipotokea nilitaka kupiga mimi mwenyewe kuendeleza nilichoahidi, saa hizi ningekuwa na mabao matatu, anayeongoza kwenye ufungaji mpaka sasa si ana mabao matano jamani? Sasa matatu si yangebaki mawili tu, tungekuwa tunafukuzana," alisema Bacca na kulalamika juu ya kukatazwa kupiga penalti na nahodha wake, Bakari Mwamnyeto.

# GONGA FC MABINGWA UMOJA CUP RORYA 2024

**Na Mwandishi Wetu,** RORYA

HATIMAYE michuano ya Umoja Cup Rorya 2024, imetamatika mwishoni mwa wiki kwa Gonga FC kutawazwa mabingwa wapya baada ya kuibuka na ushindi wa mikwaju ya penalti 7-6 dhidi ya wanafainali wenzao na mabingwa watetezi, Wanamaji FC.

**Katika mtanange huo mkali wa fainali uliopigwa kwenye Uwanja wa Maji Sota, Rorya, timu hizo zilifika hatua ya mikwaju ya penalti baada ya dakika 90 za mchezo kutamatika kwa sare ya mabao 2-2.**

Gonga FC ya Busurwa ilitinga fainali baada ya kuwatupa nje Kabwana FC kwenye mchezo wa nusu fainali wakati waliokuwa mabingwa watetezi na wenyeji wa michuano hiyo, Wanamaji fc wakiwaondosha mashindanoni Bubombi fc.

Katika mashindano hayo ya kila mwaka ya Umoja Cup Wilaya ya Rorya ambayo yalianza tangu mapema Agosti mwaka huu na kujumuisha timu 18 kwa mfumo wa makundi, yalishuhudiwa pia timu ya Kabwana FC ikiibuka mshindi wa tatu baada ya kuitoa Bubombi FC.

Kwa kutwaa ubingwa huo Gonga FC imeondoka na kitita cha shilingi 500,000, seti moja ya jezi na kombe, huku Wanamaji FC wakitia kibindoni Sh. 200,000 na seti moja ya jezi kwa kumaliza nafasi ya pili.

Kabwana FC nayo ilizawadiwa seti moja ya jezi na Sh.100,000, kwa kushika nafasi ya tatu huku wanyonge wao, Bubombi FC wakiondoka na jezi seti moja na Sh. 50,000 kwa kushika nafasi ya nne.

Aidha, Thomas John alitangazwa kuwa Golikipa Bora wa mashindano hayo na kuzawadiwa Sh. 30,000 huku Mfungaji Bora akiwa ni Riziki Abega wa Wanamaji FC naye akiondoka na kitita kama hicho wakati Mchezaji Bora, Victor Simon wa Kabwana FC yeye akizawadiwa Sh. 40,000.

Mchezaji Bora Chipukizi, Yohana Masha wa Young Boys yeye alizawadiwa Sh. 20,000 huku Kocha Bora, Ochieko Bora wa Gonga FC akipewa zawadi ya Sh. 50,000 wakati Nyakina FC ilitangazwa kuwa timu yenye nidhamu na kuzawadi Sh. 30,000.

Mbali na zawadi hizo pia timu zote zilizoshiriki michuano hiyo mwaka huu, kila moja ilizawadiwa mpira mmoja.

Katika hatua nyingine, mdhamini wa michuano hiyo kwa zaidi ya miaka 11, Peter Owino, alitunukiwa cheti kutoka Chama cha Soka Wilaya ya Rorya (ROFA), kwa kutambua mchango wake uliotukuka wa kuendeleza na kukuza soka wilayani humo.

"Tunatoa pongezi za dhati kwa waandaaji wa mashindano ya Umoja Cup, wamejitahidi sana kufanya mashindano kuwa na utofauti kila mwaka, hongereni sana, hongera sana kwa mdhamini wa Umoja Cup [Peter Owino], Mwenyezi Mungu akupe maisha marefu kwa ajili ya furaha ya Wanaumoja Cup," alisema Afisa Michezo wa Wilaya ya Rorya, Said Masanja.




Mwenyekiti wa Chama cha Soka Wilaya ya Rorya (ROFA), Jumanne Magongwe, akimkabidhi cheti Mdhamini wa Umoja Cup, Peter Owino (kulia), kwa kutambua mchango wake uliotukuka katika kuendeleza soka wilayani humo. Hafla hiyo fupi ilifanyika Jumamosi katika Uwanja wa Maji Sota, Rorya wakati wa kukabidhi zawadi kwa washindi wa michuano ya Umoja Cup 2024 ambapo timu ya Gonga FC iliibuka mabingwa kwa kuifunga Wanamaji FC kwenye mechi ya fainali. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## *Kocha JKU ashangaa Mlandege kuwafunga mabao machache*

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

KOCHA Mkuu wa JKU SC, Salum Ali Haji, amesema timu yake ilistahili kufungwa katika mchezo wao wa nne dhidi ya Mlandege FC, kutokana na kiwango walichooonesha wachezaji wake.

Mabingwa hao watetezi walikubali kichapo cha mabao 3-1 kutoka kwa Mlandefe FC mchezo uliochezwa juzi, Jumamosi katika dimba la New Amaan Complex majira ya saa kumi alasiri.

Mlandege FC huo unakuwa mchezo wao wa kwanza kupata alama tatu baada ya kutawaliwa na matokeo ya sare wakati JKU SC umekuwa wao wa kwanza kupoteza baada ya kushinda michezo mitatu mfululizo.

Akizungumza baada ya kumalizika mechi hiyo, Kocha Salum alisema walistahili kufungwa mabao mengi zaidi ya hayo waliyofungwa kutokana na mchezo wenyewe ulivyokuwa.

Alisema katika kipindi cha kwanza timu yake ilikuwa bora na ilicheza vizuri dakika zote za kipindi hicho tofauti na kipindi cha pili ambapo wapinzani wao walimiliki mpira zaidi.

Kocha huyo alisema kipindi cha pili walizidiwa katika maeneo yote na kusababisha wapinzani wao kutawala mchezo huo hadi filimbi ya mwisho ya mwamuzi.

"Ni sehemu tu ya mchezo huu haukuwa bahati yetu, tulizidiwa kila eneo, wachezaji walijitajidi kukaa katika nafasi zao, lakini walipoteana kutokana na presha ya mchezo wenyewe na mashambulizi ya mara kwa mara katika lango letu," alisema.

Michezo
Jumatatu Oktoba 7, 2024
Nipashe



**Pogba afunguka kushinda rufani** UKURASA 21



Mwekezaji na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Simba, Mohamed ‘Mo’ Dewji, akiwa na viongozi mbalimbali wa klabu hiyo, akiwasalimia wanachama wakati wa Mkutano Mkuu wa Mwaka uliofanyika jijini Dar es Salaam jana. **MPIGAPICHA WETU**

## Bacca apania kuitungua Simba

**Na Adam Fungamwango**

BEKI wa Kati wa Yanga, Ibrahim Hamad ‘Bacca’, amesema katika mwendelezo wake wa kusaka kiatu cha dhahabu, anatamani pia kufunga bao katika mechi ijayo dhidi ya Simba, Oktoba 19, mwaka huu.

Akizungumza jijini Dar es Salaam, mchezaji huyo alisema kwa sasa anatamani kufunga bao kwenye kila mchezo ambao timu yake inacheza hasa kwenye Ligi Kuu ambako ameamua kuingia rasmi kwenye kinyang’anyiro cha kuwania ufungaji bora.

Bacca, aliwashangaza mashabiki wa soka baada ya mchezo wa Ligi Kuu dhidi ya KenGold, Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya, akisema kuwa ameingia rasmi kwenye kinyang’anyiro cha kuwania ufungaji bora msimu huu.

Ilikuwa ni baada ya kufunga bao pekee kwenye mchezo huo uliopigwa uwanjani hapo Septemba 26, mwaka huu, Yanga ikishinda bao 1-0.

Ilionekana kama ni kufurahisha baraza, lakini aliwashtua wengi alipopachika

INAENDELEA UK. 23

# Simba na bajeti ya bilioni 28/-

**Na Faustine Feliciane**

## ●●● Mo Dewji aahidi makubwa, kujenga hosteli, viwanja, kurejesha makali yake, akemea…

KLABU ya Simba imepanga kutumia kiasi cha shilingi bilioni 28.4 kwa ajili ya msimu huu wa 2024-25, huku Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa klabu hiyo, Mohamed ‘Mo’ Dewji akiahidi makubwa zaidi.

**Simba jana walifanya Mkutano Mkuu wa Wanachama jijini Dar es Salaam ambapo pamoja na yote walijadili taarifa ya fedha msimu uliopita na kupitisha bajeti ya msimu wa 2024-25.**

Akitoa taarifa hiyo, Mkuu wa Kitengo cha Fedha wa klabu hiyo, Suleiman Kaumbu, alisema msimu huu wanatarajia kutumia zaidi ya shilingi bilioni 28 kwa ajili ya matumizi mbalimbali.

Suleiman alisema fedha hizo wanatarajia kukusanya kupitia vyanzo mbalimbali vya mapato ikiwamo viingilio vya uwanjani ambapo malengo yao ni kukusanya zaidi ya shilingi bilioni moja katika mechi za ligi na mashindano ya kimataifa.

“Lakini pia tunatarajia kukusanya shilingi bilioni 3.3 kwa wadhamini Simba TV, kampuni ya Azam Media, tunatarajia kukusanya milioni 480 kama haki ya matangazo, lakini pia tunatarajia kukusanya shilingi milioni 500 kutoka kwenye jengo la klabu kama kodi,” alisema Suleiman.

Aidha, akitaja vyanzo vingine, alisema wanatarajia kukusanya shilingi bilioni 1.4 kutoka kwa wanachama kama ada, shilingi bilioni 508 kama watafanikiwa kufika nusu fainali ya mashindano ya CAF, shilingi milioni 494 kwenye Tamasha la Simba Day na shilingi milioni 400 kutoka Simba App huku pia wakitarajia kukusanya zaidi ya shilingi milioni 500 kwa kuuza wachezaji.

Pia alisema wanatarajia kupata Shilingi bilioni 2.9 kutoka kwa mdhamini mkuu wa klabu hiyo, M-Bet, bilioni 1.5 kutoka kwa mdhamini wa jezi, milioni 155 mdhamini wa Ligi Kuu Benki ya NBC, milioni 500 Kampuni ya Serengeti, milioni 250 kutoka Kampuni ya A1 na shilingi milioni 250 kutoka vyanzo vingine.

Alisema fedha hizo zimeanza kutumika kwenye maeneo mbalimbali kama malipo ya mishahara kwa wachezaji, usajili, kulipa kodi mbalimbali za serikali, gharama za safari, gharama za ofisi, gharama za masoko na promosheni mbalimbali na gharama za kambi ya timu hiyo.

### Mo Dewji atoa bil. 7/-

Akiwasilisha taarifa hiyo ya fedha mbele ya wanachama zaidi ya 700 walioudhuria mkutano huo, Suleiman alisema Mwekezaji wa klabu hiyo na Mwenyeiti wa Bodi ya Wakurugenzi, Mohamed ‘Mo’ Dewji, tayari ametoa shilingi bilioni saba ambazo tayari zimeanza kutumika kwenye usajili wa klabu hiyo.

“Fedha hizi ziliwekwa kwenye akaunti ya klabu na sehemu zimetumika katika usajili wa wachezaji wapya kwenye kikosi chetu, tunamshukuru sana mwekezaji wetu,” alisema Suleiman.

### ... Aahidi makubwa

Akizungumza kwenye Mkutano huo ulioanza saa 4:26 asubuhi, Mo Dewji, alisema bado ana maono makubwa na klabu hiyo kutwaa ubingwa wa Afrika siku moja.

Alisema amerudi tena kwenye nafasi yake ndani ya klabu hiyo ili kuongeza msukumo kwenye maono yake hayo.

“Tumesajili wachezai wapya 14 akiwamo [Elie] Mpanzu, lengo ni kuona Simba inacheza soka safi na kutwaa ubingwa wa Afrika siku moja, tuna imani kubwa na benchi letu la ufundi na kwa muda mfupi mabadiliko tumeanza kuyaona, tutaendelea kubuni mifumo mipya ili Simba iweze kurejea kwenye makali yake na kufanya vizuri,” alisema Dewji.

Alisema hivi karibuni wataanza rasmi ujenzi wa majengo mbalimbali kwenye uwanja wao wa Mo Simba Arena ikiwa ni pamoja na kambi ya mazoezi, ujenzi wa hosteli, bwawa la kuogelea, ujenzi wa viwanja vitano, jengo la makumbusho ya klabu hiyo pamoja na kuanzisha akademi ya vijana.

“Tutafanya haya yote kwa sababu mchakato wa mabadiliko ya katiba upo ukingoni kabisa, tusingeweza kufanya hivi kwa sababu bado mchakato ulikuwa haujafikia mwisho, lakini kwa sasa tupo hatua nzuri na ujenzi huu utaanza hivi karibuni,” alisema Mo.

### Akemea fitna klabuni

Mo Dewji amewataka wanachama wa klabu hiyo kuacha fitna kwa viongozi na badala yake kuungana kwa pamoja kuhakikisha wanaifikisha Simba kwenye malengo yao.

“Hatutaki fitna, tukaze kamba na tuwe kitu kimoja tusigawanyike ili tufikie malengo yetu,

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042